Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

# Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 181 | DH.HIJ/ MUHAR. 1435/36 AH | OKT./NOV. 2014 | TABK/NUBW. 1393 HS | BEI TSH. 500/=

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

**Sema: Hii ndiyo njia yangu, ninaita kwa Mwenyezi Mungu kwa ujuzi hasa, mimi na wanaonifuata. Na Mwenyezi Mungu Yu mbali na kila upungufu; wala mimi simo miongoni mwa washirikina. Na Hatukutuma kabla yako isipokuwa wanaume Tuliowafunulia katika watu wa mji. ...**
**(*Yuusuf* 12:109 - 110).**

# Jalsa Salana ya 45 Tanzania

# Khalifa Mtukufu atuma salamu za kuitakia baraka

**Na Mwandishi wetu**

Jalsa salana ya mwaka huu ilipata bahati maalum ya kutumiwa ujumbe wa baraka ba Hadhrat Khalifatul masih V a.t.b.a.
Barua ya Huzur ya tarehe 09 Agosti ikiwa na kumb. No: T-3220 ilisema:
**Wapendwa Waislam wa Ahmadiyya, Jama'at ya Tanzania**

Assalam Alaikum wa rahmatullah wa barakatuhu!
Nimefurahishwa sana kwamba mnaifanya Jalsa Salana yenu tarehe 26, 27 na 28 Septemba 2014. Ni maombi yangu kwamba Mungu aibariki Jalsa yenu kupata mafanikio na awawezeshe wanajumuia wote kupata Baraka zisizo hesabika kutokana na mkusanyiko huu wa kipekee.

Natamani kuona kwamba wafuasi wa Jama'at yetu wanajitahidi wakati wote kujitakasa na kufikia viwango vya juu vya *Taqwa* ili wawe mifano bora kabisa ya Waislam Duniani. Ni muhimu kijifikiria na kukagua tabia yenu wenyewe kisha kujaribu kuboresha mwenendo na matendo yenu kila siku. Yawapasa kuwatendea watu wengine kwa wema na heshima ili kwamba muweze kuvikaribia viwango ambavyo Masihi Aliyeahidiwa (as) alivitarajia katika Jama'at hii. Maneno yenu hayana budi yafanane na matendo yenu ili mpate kuwa wawakilishi wa kweli wa Islam.
Katika siku na zama hizi, ambapo hata wasio Wa-Ahmadiyya wanatangaza kwamba wamevutiwa na mazuri ya Uislam kama yanavyobainishwa na Jumuia ya Waislam Ahmadiyyah, ambayo ndio Islam ya kweli, na ambayo inaenda sambamba na mafundisho ya Qur'an Tukufu, basi wajibu wa Muahmadiyya unaongezeka mara dufu. Kwa hiyo ni muhimu kwamba kwa kushiriki katika Jalsa hii mjitahidi kuongeza

*Endelea uk. 2*

# Watu zaidi ya 3000 wahudhuria mkutano wa mwaka 2014

## • *Wawakilishi wa serikali wasifia shughuli za Jumuiya*

**Na Mwandishi Wetu**
**Dar es Salaam**

Jalsa Salana (mkutano wa mwaka) wa 45, 2014 umemamalizika kwa mafanikio makubwa.

Mkutano huo ulifanyika kwenye siku za Ijumaa hadi Jumapili tarehe 26-28, Septemba 2014 huko katika viunga vya Jumuiya, Kitonga nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam. Watu wapatao 3000 kutoka mikoa yote nchini na nje ya nchi walihudhuria kwenye Jalsa hiyo. Wageni waalikwa kutoka serikalini, Jumuiya za kidini, Vyama vya siasa na taasisi zingine za Kijamii nao walihudhuria kwenye mkutano huo. Mkutano wa mwaka huu ulipata mafanikio makubwa kwani mbali ya kuwa na idadi kubwa ya washiriki ulihudhuriwa na wageni 9 kutoka Mozambique wakiwemo Lajna watatu.



*Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mh. Seif Rashid Suleiman akitoa hotuba kwenye mkutano wa mwak a(Jalsa Salana) ya 45, Kitonga Dar es Salaam*

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini akifungua mkutano huo alisoma salamu za Khalifa Mtukufu a.t.b.a. na kisha akawakumbusha waliohudhuria kuzingatia makusudio ya mkutano huo kama yalivyotajwa na mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya hii yeye mwenyewe.
Alisema:
" Lengo na shabaha ya Jalsa salana ni kuwajumuisha mara kwa mara wanajamaati, wakutane kuleta mabadiliko kati yao ili nyoyo zao zielekee kwenye maisha ya akhera, wapate kumwogopa Mwenyezi Mungu, wawe mifano mizuri kwa wengine katika utawa, ucha Mungu, huruma kwa wanadamu na ili uchaji Mungu upate kuongezeka katika mioyo yao ". (Ushahidi wa Qurani)
Pia alisema:
" Jalsa hii sio kama tamasha za kidunia za kulazimisha mipango yake. Bali kufanyika kwa jalsa hii kunategemea kupatikana kwa matunda mazuri, bila hivyo ni bure tu kwani faida za jalsa hii na athari zake juu ya khulka za watu lazima zionekane, bali makusudio na madhumuni ya mpango wangu ni kuwarekebisha khulka

*Endelea uk. 2*

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

# Salamu za Khalifa Mtukufu

*Kutoka uk. 1*

elimu yenu ya dini, mjaribu kuboresha hali za maisha yenu na mtekeleze kila jambo la hekima na la kiucha-Mungu mnalojifunza, na kwa namna hiyo muongeze sana ukuaji wenu kiroho.

Masihi Aliyeahidiwa (as) amesema kuhusiana na malengo ya Jalsa kwamba kwa kuhudhuria kwenye Jalsa mwapaswa kuongeza daraja lenu la *Taqwa*, yaani ucha Mungu, na kwamba mnapaswa kumwogopa Mungu. Jalsa hii inatakiwa kuwa nyenzo ya kuzalisha hofu ya kweli ya Mwenyezi Mungu ndani ya nyoyo zenu. Inatakiwa isababishe upole, wema na hali ya amani kuzalika ndani yenu na kufanya mapenzi yastawi baina yenu, kwa wingi, kiasi kwamba muwe mfano wa udugu kwa wote wawaonao. Yawapasa kuanzisha mfano wa kudumu wa kujaliana. Yawapasa kuzalisha unyenyekevu na upole katika nyoyo zenu. Zaidi ya yote, yawapasa kuzalisha jazba na hamu ya kuitumikia imani na jaribuni kuanzisha mahusiano yaliyo hai na Allah, Mwenye Enzi.

Kwa hivyo, nawahimizeni muanzishe uhusiano wa karibu na Allah mwenye enzi na muifanye ibada Yake kuwa ni lengo la maisha yenu. Qur'an Tukufu imesema kwamba lengo hasa la maisha ni kumwabudu Allah na kupata ukaribu Nae. Njia bora kabisa ya ibada ambayo Qur'an Tukufu imefundisha ni Salat. Kwa hiyo kila Mu-Ahmadiyya anatakiwa ajipange kusali sala zake tano za siku kwa wakati na kwa Jamaa.

Masihi aliyeahidiwa (as) anasema juu ya hili:

*"Nakwambieni tena kwamba kama mnataka kuanzisha mahusiano ya kweli na Allah, ishikilieni vyema Salat kwa namna ambayo miili yenu na ndimi zenu na tamaa zenu zote za kiroho na jazba zenu zipate kuwa dhihirisho la Sala". ( Malfoozat Jalada 1 uk. 170)*

Anaongeza kusema:

*"Kwa hiyo sikilizeni nyote ninyi mnaojitambua kuwa wa Jumuia yangu; Pale tu mtakapoenenda katika njia ya uchaji Mungu ndipo hapo tu mtakapohesabiwa mbinguni kuwa ni wa Jumuia yangu. Kwa hiyo salini Sala zenu mara tano kwa siku mkiwa katika msisimko wa hofu na ufahamu wa kuwapo kwa Mwenye enzi Allah kama vile mnamuona kwa macho yenu". (Roohani Khaza'een Jalada la 20 uk.307)*

Kwa hakika mna bahati njema sana kumtambua Imam wa zama na kumkubali kuwa ndiye Masihi Aliyeahidiwa (as). Yawapaseni kwa hiyo kushikilia kiapo cha utii mlichokifanya kwenye mkono wake. Nyoyo zenu hazina budi kufurahika kwa kuwa baada yake (Masih as), Allah hakukuacheni bali amewafadhilini kwa baraka ya mara kwa mara ya Ukhalifa ambao umeendelea kutolewa kwa wana-Jumuia kwa zaidi ya miaka 105 (sasa).

Nawahimizeni kusikiliza wakati wote Hotuba zangu za Ijumaa pamoja na maelekezo na Hotuba zangu zingine. Hii itawawezesheni kuimarishika mshikamano na utii wenu kwa taasisi ya Ukhilafa. Mnapaswa pia kuwafundisha watoto wenu juu ya Baraka maalum za taasisi ya Ukhalifa na kuwahimiza kudumu wameshikamana nao, na kuwa siku zote watiifu kwa Khalifa wa zama. Leo hii, kazi ya kuhuisha Islam inaweza tu kufanywa kwa kushikamana na mfumo wa Ukhalifa. Kwa hiyo, inatakiwa daima mjitahidi kuienzi taasisi hii adhimu na kuhakikisha nyinyi na vizazi vyenu vijavyo, siku zote mnabaki katika mwongozo wenye baraka na hifadhi ya Khilafat-e-Ahmadiyya. Allah awawezesheni kufanya hivyo.

Nataka pia kuwakumbusheni wajibu wenu juu ya mahubiri. Tabligh ni lazima kwa kila Muislam Ahmadiyya na mfano wenu mwema ni wa lazima ili kupata mafanikio katika juhudi zenu za Tabligh. Kwa hiyo kama matendo yetu yataoana na mafundisho ya Islam na kila neno na tendo letu litaenda sawa na mafundisho ya Qur'an Tukufu, na yatakuwa katika umbo na hali ambayo Masihi Alieahidiwa (as) ametamani kwa ajili yetu, basi hii itakuwa ni nyenzo kubwa ya kupeleka ujumbe wa Islam Ahmadiyya kwa watu wa nchi yenu kimahsusi na Dunia kwa ujumla. Allah na awabarikini wote!.

Wasalam,

Wenu Mwaminifu,

Imesainiwa

**Mirza Masroor Ahmad**
**KHALILIFATUL MASIH V**

# Watu zaidi ya 3000 wahudhuria

*Kutoka uk. 1*

zao, watu waondokane na maovu, wawe watu wema na wa Mungu ". ( Ushahidi wa Qurani ).

Amir na Mbashiri Mkuu aliendelea kuwakumbusha wanajumuiya na wote waliohudhuria mkutano huo kuwa wazingativu katika siku zote tatu za mkutano na kuhakikisha kwamba wanashiriki kwenye taratibu zote zilizopangwa ili kuweza kufaidika kikamilifu na mkutano huo.

Katika mkutano huo mada mbali mbali zilitolewa na wataalamu wa Jumuiya. Mada hizo ni pamoja na:

'Umuhimu wa kuziamini na kuzitumainia sifa za Mwenyezi Mungu katika maisha yetu ya kila siku' iliyotolewa na Sh. Asif Butt wa Morogoro:

Mada pili ni 'Nafasi ya Qur'ani tukufu katika maisha ya kila siku ya mwaminio' iliyotolewa na Mwl. Shamuni Juma wa Jamia Ahmadiyya Morogoro wakati ambapo mada ya tatu ilikuwa ni 'Mfano bora wa Mtukufu Mtume s.a.w. katika maisha ya ndoa na juu ya malezi ya watoto' iliyotolewa na Sh. Riaz A. Dogar wa Iringa.

Mada ya nne ilikuwa ni 'Umuhimu na baraka za Ukhalifa katika zama hizi' iliyotolewa na Sh. Waseem Khan wa Tabora wakati mada ya tano ilihusu 'Maisha ya Maulana Dr. Abdulwahab Adam wa Ghana ambaye alifariki mwaka huu iliyotolewa na Dr. Swalehe Kitabu Pazi wa Dar es Salaam.

Mada ya sita ambayo ilitolewa na Katibu Mkuu wa Jamaat Ahmadiyya nchini Bw. Seif Hassan Nakuchima ilihusu Baraka za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika kuharakisha ufikishaji wa ujumbe wa Allah (Tabligh) na upatikanaji wa malezi kwa waaminio (Tarbiyyat) na mada ya saba ikawa Mwenendo mwema unaotarajiwa kwa kila Ahmadiyya baada ya kufanya baiat kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. iliyotolewa na Sheikh Bakri Abedi wa Morogoro

Mada ya nane ilikuwa ni Wajibu wa kila Ahmadiyya katika kuchangia maendeleo ya Jamaat nchini iliyotolewa na Mwl. Abdullah Mbanga na mada ya mwisho ilikuwa ni Jinsi Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. alivyowatendea kwa wema wasio Waislamu iliyotolewa na Mwl. Abdulrahman Ame.

Kama ilivyo kawaida ya Jalsa salana zetu, Wageni kadhaa wa serikali na wawakilishi wa Jumuiya za kidini, viongozi vya vyama vya siasa na wale wa kijamii katika ngazi mbalimbali walialikwa kwenye mkutano huo.

Miongoni mwa walioalikwa na kuhudhuria katika mkutano huo ni Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mh. Seif Rashid ambaye alihudhuria kwenye siku ya kwanza ya mkutano huo. Wengine waliohudhuria ni Mh. Januari Makamba Naibu Waziri wa Sayanasi na Teknolojia na Mh. Rymond Mushi Mkuu wa Wilya ya Ilala Dar es Salaam ambaye alikuja kumwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salama ambaye naye alikuwa aje kumwakilisha Mh. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakiongea kwa nyakati tofauti sawa na vipindi vyao walivyoalikwa viongozi wote walipongeza msimamo wa Jumuiya kusimama kwenye kauli mbiu ya Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote na wakasema kwamba hiyo ni kauli inayostahili kuigwa na wengine. Wakasifia kwamba kwa kushi kwa kauli hii Jumuiya imeendelea kuwepo hapa nchini kwa kipindi kirefu lakini hakuna kumbukumbu zozote serikalini zinazoonesha kwamba Jumuiya imewahipo kusababisha au kuwa chanzo cha vurugu lolote ndani ya nchi.

Wakasifia pia utaratibu wa Jumuiya wa kutokujiingiza kwenye mambo ya siasa na badala yake kuwahimiza watu wake kuwa watii kwa serikali yoyote iliyopo madarakani na kwamba hilo ni jamob muhimu katika kulinda amani ya jamii na taifa lolote na katika kuhakikisha kwamba wananchi wanajiletea maendeleo yao.

Vile vile wakiongelea kwa nyakati tofauti juu ya msimamo wa serikali yetu wa kutokuwa na dini maalum ya serikali na badala yake kuwaacha wananchi wake kuchagua dini wazipendazo waliahidi kwamba serikali itaendelea na msimamo huo kwani ndio msimamo pekee unaohakikisha kuwa kila mtu anakuwa huru kuabudu kupitia dini aipandayo.

Pia waliziipongeza Jumuiya za kidini nchini katika juhudi zao za kusaidi katika huduma za kijamii na kuipongeza Jumuiya hasa kupitia miradi kadhaa ya maji na afya iliyotekelezwa hapa nchini kwa kiindi cha miaka michache iliyopta. Huduma hizo ni pamoja na utoaji wa mashine za mammogramu kwa hospitali ya taifa ya Muhimbili, uchimbaji wa visima vya maji safi kwenye maeneo kadhaa nchini kamoja na ugawaji wa vifaa vya kielimu kwa shule kadhaa hapa nchini.

Washiriki wa Mkutano wa mwaka huuu wamesifia uboreshwaji kadhaa uliofanyika kwenye Jalsa na wengi wao wamesema kwamba maendeleo ya Jalsa yanawazidishia imani yao juu ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwani wakati ambapo Jalsa ya kwanza iliyofanyika mwaka 1891 huko Qadiani India ilihudhuriwa na masahaba 75 tu, leo Jalsa zinahudhuriwa na maelfu ya watu katika nchi mbalimbali kama ilivyotabiriwa na Masihi Aliyeahidiwa mwenyewe.

Hapa nchini petu tumekuwa tukishuhudia mabadiliko mbalimbali juu ya kuboreka kwa Jalsa Salana mwaka hadi mwaka.

Mwenyezi Mungu Atusaidie ili Jalsa yetu iendelee kufikia lengo lake ililokusudiwa.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

# Jinsi Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. alivyowatendea kwa wema wasio Waislamu.

*Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2014 na Mwl. Abdulrahman M. Ame*



*Nasiratul Ahmadiyya wakisoma shairi kwenye Jalsa Salana ya mwaka huu 2014*

Wanadamu leo, tunaishi kwenye dunia yenye changamoto nyingi sana. Ziko changamoto za kijamii, kisiasa, kiuchumi, n.k. lakini hizo zote ukizichunguza hasa ni zao la changamoto za kidini. Kwenye dini, wakati kwa upande mmoja uelewa wa dini pamoja na maana ya kweli ya roho ya dini ukiwa unaendelea kufifia na kufutika kwenye nyoyo za wanadamu, wengi wa watu wakiwa wanafuata dhana zao tu na wala sio mafundisho ya kweli ya dini zao, kwa upande mwingine kumezuka wimbi kubwa la watu wenye misimamo mikali ya kidini, wasio tayari kuvumilia kuishi pamoja na watu wa imani zingine na pengine wasio tayari hata kuishi pamoja na watu wa imani zao wenyewe madamu tu watakuwa wanatofautiana nao kimawazo kwenye mambo madogo tu. Kudhani kwamba kila asiyekubaliana nawe kiimani ni adui na dawa yake ni kumuuwa inaonekana ndio ugonjwa mbaya na wa hatari unaondelea kuitafuna jamii ya wanadamu leo.

Kwa mfano wako baadhi wa waislamu wadhanio kwamba haifai kushirikiana na asiye mwislamu katika hali yoyote iwayo. (kwa maana nyingine hawajui ni mahusiano gani yanatakiwa yawepo kati ya muislam na asiye mwislamu) bali kwao wao asiye mwislamu hana haki sio ya uhuru wa kuabudu sawa na imani yake tu bali hata hana haki ya kuishi!.

Kwa upande mwingine baadhi ya wasio waislamu nao ama kwa kuona mifano hii mibaya ya baadhi ya waislamu au nao kwa uelewa wao binafsi usio sahihi juu ya uislamu nao wanaudhani uislamu kuwa ni dini ya fujo, isiyo na subira wala uvumilivu bali isiyohimili vishindo vya kuishi na watu wa imani vingine; na bila shaka lawama zao nzito mwishowe wanazitupa juu ya uso mng'aavu na uliobarikiwa wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w.

Mada niliyopangiwa basi, imekusudiwa kutoa mwanga juu ya hili: Ni yepi hasa yalikuwa mahusiano ya Mtukufu Mtume s.a.w. kwa wasio waislamu au kwa maana nyingine Mtukufu Mtume s.a.w. aliwatendea namna gani wasio waislamu, ili nasi tukiwa wafuasi wa Mtume huyu aliye Mbora wa Manabii tuweze kuiga mifano na mwenendo wake na ili tuweze kuona wajibu tulionao wa kuishi pamoja na watu wa dini na imani zingine kwa amani.

Wasikilizaji wapendwa, tuyaangaliapo maisha ya Mtume s.a.w. tunayakuta kwamba ni maisha ya mtu mwenye mawazo mapana sana yaliyofurika mifano lukuki ya unyenyekevu, upole, subira, uvumilivu, kuishi kwa amani na watu wa dini zingine, kujali mapungufu ya wengine, kutenda kwa haki na adili bila kujali mipaka ya udugu, kabila au dini, n.k. n.k. ikithibitisha kauli ya Allah: ***Wainnaka la'ala khuluqin adhiimu:***

Na bila shaka una tabia njema, tukufu (68:5).

Maisha ya Mtukufu Mtume s.a.w. kama ilivyowekwa na Hadhrat Musleh Mauud r.a. "ni kitabu kilicho wazi" - kilichojaa mifano mingi mno ya wema usio na mfano, ukarimu, huruma, kusaidia wengine, kusamehe makosa ya wengine, n.k. n.k. sio kwa wafuasi wake tu, bali kwa wale pia waliokataa kuamini ujumbe wake lakini hata kwa wale waliokuwa wapinzani au waliojifanya maadui zake wakubwa na ambao hawakuacha hata nafasi moja iliyopatikana ya kumfuta yeye na ujumbe wake bila kuitumia - hao pia walikula na kushiba matunda ya sifa zake hizo. Ni kweli, amesema kweli, Yule aliye Mbora wa wasema kweli, Allah Subhaananu Wataala Aliposema: ***Wamaa arsalnaaka Illaa Rahmtan Lilialamiin***

Nasi Hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu (21:108).

Wasikilizaji wapendwa;

Bila shaka nyote mtakumbuka kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. alipitia safari ya ndefu ya maisha yake kwenye hali za aina mbali mbali ili uwe mfano kwa kila mtu.

Hata kabla ya kupewa utume Mtukufu Mtume s.a.w. alishaonyesha sifa nyingi za wema, ukweli, uaminifu, kuchunga ahadi, kusaidia wengine – hasa wanyonge na wenye kuonewa n.k. – bila ya ubaguzi wowote - kiasi hiki kwamba wakazi wote wa Makka walimpa lakabu ya *Aswadikul Amiin* – Mkweli Mwaminifu.

Mtukufu Mtume s.a.w. aliendelea kuzishikilia sifa hizi katika maisha yake yote na kamwe hakubadilika hata kama watu wake walimbadilikia, aliendelea kushikilia ukweli na uaminifu, aliendelea kusaidia wanyonge na wenye kudhulumiwa bila kujali tofauti zao za kiimani.

Tukio la mgeni aliyefika mjini Makka akiomba msaada kwa watu ili alipwe deni analomdai Abu Jahal unatosha kuonyesha msimamo wake ulikuwaje mahala palipohitaji kusimamia haki na adili. Bila kumjali adui yake mkubwa Abu Jahali na bila kuangalia kwamba anayedai ni mtu wa imani gani au ni mtu wa kabila gani, Mtukufu Mtume s.a.w. alipojiwa na mtu huyo kumuaomba msaada baada ya kuwa amekosa msaada kwa wakazi wote wa Makka hakusita hata kidogo kumsaidia. Wakazi wa Makka wakitaka kumuabisha Muhammad ambaye walikuwa wanajua kwamba ni mwanachama mwaminifu wa kikundi kilichokula kiapo cha kuwasaidia wenye kudhulumiwa, walimtomeza mgeni huyo kwa Mtume ili kama mtume atakataa kumsaidia wapate cha kumlaumia kwamba amevunja ahadi ya kiapo chake na kama ataamua kumsaida dhana yao ilikuwa kwamba atapokea matusi kama sio kipigo kutoka kwa Abu Jahal. Lakini kumbe walikuwa hawajamjua Muhammad ni nani na anazo sifa gani. Kwa uimara wa ajabu kushinda simba, Mtukufu Mtume s.a.w. alimkabili Abu Jahali na kumuuliza je unamjua mtu huyu, Abu Jahal akajibu ndio. Je ni kweli anakudai? Abu Jahal hakuwa na jibu jingine zaidi ya kusema ndio, basi mlipe fedha yake alisema Mtume Mtukufu s.a.w. Abu Jahal bila kusema neno akaingia ndani na kutoka na kitita cha fedha na kumkabidhi mdeni wake.

Tukio jingine nalo linafaa kutajwa kuzidi kukozesha hoja hii kwamba uadui wa watu kamwe haukumfanya Mtukufu Mtume s.a.w. asite kutoa msaada au apoteze subira na uvumilivu. Akiwa kwenye mahangaiko ya mahubiri mjini Makka Mtukufu Mtume s.a.w. jioni moja alikutana na bibi mmoja kikongwe akiyoyomea nje ya mji kuelekea sehemu fulani. Akamuuliza anakwenda wapi muda kama ule, bibi akajibu, nakimbia mji huu kwani kuna mchawi anayeitwa Muhammad anawapoteza watu kwa uchawi wake, basi nami kabla sijakutana naye akaniroga kwa uchawi wake ni vyema nimkimbie. Bila ya kutoa maelezo yoyote Mtume s.a.w. akamuomba amsaidie mzigo wake, bibi akakubali na akafuatana naye hadi mwisho wa safari yake. Mtukufu Mtume s.a.w. Akamkabidhi mzigo wake na akageuka kwenda zake. Akiwa anaondoka bila kusema neno lolote, bibi akamuuliza, ewe mtu mwema wewe ni nani? Angalau niambie jina lako basi kwani sijapata kuona mtu kama wewe kwenye mji huu. Mtume s.a.w. akamjibu kwa unyenyekevu na hesima: Mimi ndiye yule mtu ambaye kwa sababu yake umeamuwa kuukimbia mji. Mimi ndiye Muhammad. Bibi kwa mshangao wa ajabu akasema kama kweli wewe ni mchawi basi umeshaniroga kwa uchawi wako na kama kweli ni mtume wa Mungu basi ninakubali ukweli wako na - bibi akasilimu.

Katika siku za mwanzo za utume wake wakazi wengi wa mji wa Makka waliamua kumfanyia kila vitimbi na dhuluma, kumuekea vinyesi na miba njiani, kumtupia matumbo machafu ya wanyama, kumrushia mawe na michanga akiwa nyumbani mwake n.k. lakini hayo yote hayakumfanya apoteze mizania bali daima alibaki akiwa mvumilivu na mwenye subira huku akiwatakia mema wapinzani wake bali siku zote kuwaombea dua. Tukio la kwenda kumuangalia yule mtoto ambaye kila siku alikuwa na tabia ya kumtupia uchafu mlangoni mwake, lakini siku ambayo hakukuta uchafu akapata hofu huyu mtoto anaumwa au la. Alipokwenda kumuangalia na kumkuta anaumwa alimuombea dua apate afya njema. Ingawa tukio hili laweza kuonekana dogo lakini linatosha kuonesha tabia ya Mtukufu Mtume s.a.w. ya subira na uvumilivu juu ya hata wale waliomfanyia kila maudhi.

Safari ya Twaif ya Mtukufu Mtume s.a.w. kwa ajili ya mahubiri ni tukio jingine linaloonesha subira na uvumilivu alikokuwa nao pamoja na kuwatakia wema wanadamu bila kujali dini yao wala upinzani wao. Baada ya kuona wakazi wa Makka wameendelea kumpinga na kuweka vidole vyao masikioni mwao Mtukufu Mtume s.a.w. alimua kufanya safari ya kwenda mji mwingine mkubwa wa jirani wa wakati huo Twaif. Alipofika huko na baada ya kuwaona wakubwa wa mji akiwaeleza lengo la kufika kwake mjini hapo na kuanza kuwahubiri, wakazi wa mji huo wote waliamua kumfukuza na wakawaagiza watoto wahuni wa mji wampige mawe hadi nje ya mji huo kiasi hiki kwamba viatu vyake vikaroa damu. Walipoamua kumuacha, akiwa taabani na akiwa amepumzika chini ya mti akivuta pumzi, Malaika Jibril alimjia na kumueleza kwamba ametumwa na Mwenyezi Mungu aamue iwapo mji ule uangamizwe kwa kugandamizwa baina ya milima mwili? Kauli yake ilikuwa ni hii tu *Laa*, hapana bali Mwenyezi Mungu awajaalie wakazi wa mji huo kama sio wao basi kizazi chao kije kiukubali na kuusaidia Uislam. Na hivyo ndivyo ilivyotokea.

Hali ilipofikia kilele cha ubaya na kutokuvumilika mjini Makka Mtukufu Mtume s.a.w. aliwaagiza wafuasi wake wahamie Uhabeshi Abysinia au Ethiopia ya leo naye mwenyewe akahamia Madina kwa amri ya Mwenyezi Mungu wakati ulipowadia. Akiwa safarini na baada ya kumtafuta kwa kufuata nyao na wakamkosa, makafiri wa Makka waliwatuma watu kadhaa mahiri wa kazi kumtafuta kwa udi na uvumba na Abu Jahal akatangaza zawadi ya ngamia 100 kwa yeyote atakayemleta Muhammad ama akiwa mzima au akishindwa kumbeba basi hata kichwa chake. Suraqa bin Malik r.a. aliyekuwa chifu wa mabedui wakati huo - na mmoja wa wataalamu wa siku hizo wa kazi hii alijitoma na akamfuatilia Mtukufu Mtume s.a.w. na rafiki yake Hadhrat Abubakar r.a. kwa utaalamu mkubwa. Baada ya safari ya ndefu akawaona, akiwakaribia ngamia wake akazama kwenye mchanga. Baada ya kujikakamua akaweza kuchomoka akawafuatilia tena na yeye na farasi wake wakazama tena kwenye mchanga. Akishindwa kujisaidia baada ya kuzama mara ya tatu, akawaomba wale anaowafukuzia kuwakamata wamsaide kumuokoa. Badala ya kumuacha afie jangwani au kuamua kuchukua nafasi

***Endelea uk. 4***

# Alivyowatendea kwa wema wasio Waislamu.

*Kutoka uk. 3*

hiyo kummalizia hapo hapo na hata baada ya kupata ushauri kutoka kwa Abubakar kwamba kwa nini 'tumsaidie mtu anayetutafuta atuue'. Mtukufu Mtume s.a.w. alimshawishi wamsaidie kumuokoa. Kikubwa alichokitaka Mtume s.a.w. kwake ni ahadi tu kwamba watakapomsaidia atarudi Makka na ataamua kukaa kimya. Lakini Suraqa hakukatwa hata ukucha, na bila shaka tukio hilo likawacha athari kubwa moyoni mwake na baadae akaamua kusilimu.

Alipofika mjini Madina Mtukufu Mtume s.a.w aliikuta jamii ya mji huo ikiwa kwenye migogoro ya magomvi, kutokuaminiana na hatari za uvunjifu wa amani zilizoenea kila kona ya mji.

Mtume s.a.w. kwa kuona hatari hizo akang'amua mwanzoni tu juu ya haja ya kaundikishiana makubalino ya amani. Makubaliano ambayo hadi leo yanawaacha hoi wapigania haki za binadamu duniani juu ya uwezo wa ajabu wa mtu huyu mtukufu. Kwa sababu ya muda sitousoma mkataba huo lakini kwa ujumla uliweka misingi ya kuishi kwa amani baina ya dini tatu zilizokuwepo Makka wakati huo. Uyahudi na Ukiristo zikiwepo tangu zamani na Uislamu ambao ulikuwa bado ni dini mpya. Kwa ujumla mkataba huu unaonesha kwamba siku zote Mtukufu Mtume s.a.w. aliliweka suala la kuishi kwa amani, uhuru wa kuabudu, usawa, haki na adili baina ya wanajamii wenye kuamini dini mbalimbali kuwa ni la kipaumbele na la umuhimu mkubwa.

Mkataba wa amani ambao Mtukufu Mtume s.a.w. aliuandikisha kwa ajili ya jamii ya Kikristo ya Mtukufu Mtume s.a.w.. Catherine ya Mlima Sinai mnamo mwaka 628, sawa na mwaka wa 6 Hijria bila shaka ni ushahidi ulio wazi wa jinsi Mtukufu Mtume s.a.w. alivyokuwa na hamu kubwa ya jamii za dini mbalimbali kuishi kwa amani na mashirikiano na kuheshimiana. Kwa vyovyote ni mkataba usio na mfano wake katika historia ya mwanadamu. Baadhi ya sehemu za mkataba huo zinasomeka:

Huu ni mkataba ambao Muhammad bin Abdullah, Mtume wa Mungu, Muonyaji na mtoaji wa bishara njema ameuandikisha ili kwamba kusibakie hoja yoyote kwa wale watakaokuja baadae. Nimeuandikisha mkataba huu kwa ajili ya Wakristo wa mashariki na magharibi, kwa wale wanaoishi karibu yetu na kwa wale wanaoishi mbali nasi, kwa ajili ya Wakristo wanaoishi leo na wale watakaokuja baadae na pia kwa wale Wakristo tunaowajua na kwa wale tusiojuana nao.

Muislamu yoyote atakayevunja yaliyomo kwenye mkataba huu atahesabiwa mwenye kuvunja agano la Mungu na muasi dhidi ya ahadi Yake (Mungu) na kwa kufanya hivyo atajichumia ghadhabu za Mungu, na ni sawa tu mtu huyo awe ni mfalme au raia wa kawaida.

Mchungaji yeyote hatofukuzwa kutoka kwenye uchungaji wake, wala Askofu hatoondolewa kutoka kwenye Uaskofu wake, hakuna Padri atakayefukuzwa kutoka sehemu yake ya ibada na hakuna hujaji atakayezuiliwa kutimiza safari yake ya kuhiji (mahala anapopaamini kuwa patakatifu).

Hakuna kanisa hata moja au sehemu yoyote ya kuabudia itakayofilisiwa, kuharibiwa au kuvunjwa. Mali au kifaaa chochote cha kanisa hakitotumika kwa kujengea msikiti au makazi kwa ajili ya waislamu; na muislamu yoyote atakayefanya kinyume na agizo hili atahesabiwa kuwa mpinzani wa Mungu na Mjumbe wake.

Watawa na Makasisi hawatalazimika kulipa jizya wala ushuru, iwe wanaishi sehemu za misituni au mitoni, au mashariki au magharibi au kaskazini au kusini. Ninawapa neno langu la kuwaheshimu. Wako kwenye ulinzi wangu na ahadi yangu na watapata kinga kamili kutokana na bughudha yoyote. Kila aina ya msaada utatolewa kwao kwa ajili ukarabati wa makanisa / majengo yao ya ibada.

Hawatolazimika kuvaa silaha kwa ajili ya ulinzi. Watalindwa na waislamu.

Basi naiwe hivi kwamba mkataba huu usivunjwe hadi siku ya hukumu.

*Umesainiwa na Muhammad Mtume wa Allah.*

Tukio jingine linaloonyesha heshima na uhuru wa kuabudu ambao Mtukufu Mtume s.a.w. aliwapatia watu wa dini zingine ni hili. Akiwa mjini Madina alifikiwa na msafara wa Wakristo kutoka Najiran .... walifika muda wa Alasiri na baada ya maongezi fulani wakaonekana kuhamanika. Mtume s.a.w. akawauliza kumetokea nini. Wakamjibu wanataka kutafuta sehemu wamuabudu Mola wao. Mtume s.a.w akawaambia hawana haja ya kuhamanika, watumie tu msikiti wake kwa ajili ya ibada yao na akawaagiza masahaba zake watoke nje na yeye mwenyewe akatoka akiwaambia waabudu kwa utulivu bila kubughudhiwa hadi watakapomaliza ibada yao wapendavyo.

Sambamba na agizo la Mwenyezi Mungu la kuwataka waislamu kuheshimu imani na njia za ibada za watu wengine Mtukufu Mtume s.a.w. siku zote alikuwa makini kuhakikisha kwamba haumizi hisia za watu wa dini zingine na siku zote anaonesha heshima juu ya imani yao.

Tukio la myahudi mmoja aliyelumbana na mwislamu fulani juu ya nani ni bora kati ya Mtukufu Mtume s.a.w. na nabii Musa linatosha kuonesha jambo hili.

Ilitokea hivi kwamba myahudi mmoja kufika kwa Mtukufu Mtume s.a.w. akilalamika kwamba ameumizwa hisia zake na mwislamu mmoja aliyeendelea kushikilia kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. ni mbora kuliko Mussa. Akimsihi Mwislamu yule, pamoja na kujua kwa hakika kwamba yeye ndiye mtume bora wa mitume wote, Mtukufu Mtume s.a.w. s.a.w. alimwabia

*Laa tufadhiluuni a'laa Musa.*

Akikusudia kwamba mbele ya waumini wa manabaii wegine hakuna haja ya kutangaza ubora wake hasa iwapo katika mjadala kwani jambo hilo litaumiza hisia zao.

Kisa cha bedui mmoja nacho chafaa kutajwa hapa ili kuzidi kukozesha rangi juu ya heshima ya ubinadamu aliyokuwa nayo Mtukufu Mtume s.a.w. bila kujali imani ya mtu na pia jinsi alivyowavulia wenye mapungufu. Bedui huyu hakuwa muislamu wakati huo, alikuja mjini Madina kwa maneno ya vijana wa kileo *'kuja kushangaa kituko kilichozuka mjini'*. Akaingia msikitini kusikiliza kinachoendelea. Akiwa amebanwa na haja ndogo akaamua kuelekea pembe moja ya msikiti kwa ndani na kuanza kujisaidia hapo hapo. Masahaba wakashituka kwa ushamba huo uliovuka mipaka na wakataka kumtimulia mbali nje. Mtukufu Mtume s.a.w. akawaambia wamwache tu hadi amalize haja yake. Na baada ya hapo, badala ya kumkaripia yule bedui au kumtaka akachote maji kuja kusafisha akawagiza masahaba zake kwamba walete maji na kumwagia sehemu hiyo. Ona heshima ya ubinadamu aliyoionesha Mtukufu Mtume s.a.w. na kuwasamehe wengine. Sijui hali ingekuwaje kwa ndugu zetu wa leo ambapo katika baadhi ya misikiti nimewahi kuona maandishi yaliyoandikwa ukutani *'zima simu yako ili usalimike'*. Pengine ikimaanisha kwamba kama itatokea simu yako itoe mlio msikitini hata kama wewe ni mgeni ambaye hujawahi kuliona tangazo hilo au umeghafilika na ukajisahau kuna hatari ya kupokea kipigo cha mwizi wa mtaani.

Wapenzi wasikilizaji, kama tujuavyo kwamba; Makafiri wa Makka hawakuridhika na kuhama kwa mtume s.a.w. na wafuasi wake kutoka Makka bali waliendelea kufanya fujo na wakasafiri hadi Madina, wakauwa watu, wakaharibu mazao, wakauwa mifugo n.k. lengo lao kubwa likiwa kuwashinikiza wenyeji wa Madina *'waifukuze nuhusi'* iliyowafikia ambayo itawasababishia kushambuliwa wakati wowote.

Ilipofikia hapo Allah akawaamuru waislamu wapigane kwa ajili ya kujitetea.

Vita vya kwanza vikawa ni Badri ambavyo waislamu walipata ushindi mkubwa, vikafatiwa na vita vya Uhud na baadae Khandak ambavyo sio tu viliwapatia waislamu ushindi mkubwa bali pia wakakamata mateka wengi. Lakini la ajabu na lililowashangaza hata masahaba wengi ni hili kwamba Mtume s.a.w. alitoa maagizo makubwa na mazito juu ya kuwatunza mateka hao na akaagiza kwamba asiye na uwezo wa kuyatimiza ni vyema asichukue mateka.

Kwa ujumla Mtukufu Mtume s.a.w. aliagiza mateka kufanyiwa kwa wema na ubinadamu mkubwa. Alisema hakuna ruhusa ya kuwaadhibu, kuwatesa, kuwapiga, kuwabebesha mizigo au kuwafanyisha kazi wasiyoiweza n.k. Aliagiza kwamba hakuna ruhusa ya hata mwanamke mmoja kuguswa na mateka wote wapatiwe chakula kabla ya wanaowachunga hawajakula, na wapatiwe mavazi kabla ya wanaowachunga hawajavaa. Wale walioweza kujikomboa kwa mali zao walipatiwa nafasi ya kujikomboa. Wale waliokuwa na fani zao kama vile ualimu, ufundi n.k. wakapewa mapatano ya kujikomboa kwa kuwahudumia Waislamu kwenye fani zao kwa kipindi fulani. Wenye kujua kusoma na kuandika waliwasomesha waislamu, wajenzi walisaidia kujenga na mapatano yalipotimizwa tu wakapewa uhuru wao.

Kwa upande mwingine Mtukufu Mtume s.a.w. aliagiza mateka wote wafanyiwe kwa adili na usawa na kamwe ukaribu na ujamaa usitumike kama kipimo cha kuwakandamiza wengine na kuwasaidia wengine. Akiwa anarudi mjini Madina kutoka kwenye moja ya vita hivyo huku wakiwa wamebeba mateka na mmoja wao akiwa ni mjomba wake Mtukufu Mtume s.a.w. Hadhrat Abbas r.a. Bwana huyu aliendelea kupiga makelele safari nzima na kwa sababu ya kelele hizo Mtukufu Mtume s.a.w. hakupata utulivu wa kulala na mara kadhaa akawa anatoka kutoka kwenye hema yake na kuchungulia.

Kwa kuona hivi masahaba waliopewa kazi ya kuwalinda mateka hao wakadhani kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. anapata huzuni inayomnyima usingizi kwa sababu ya mjomba wake huyo na hivyo wakaamua kuilegeza kamba aliyokuwa amefungwa ili apunguze kulalama. Kwa kipindi fulani Mtukufu Mtume s.a.w. akasikia kimya, lakini kwa mshangao wa masahaba badala ya kulala akaja tena kuchungulia na kuuliza kumetokea nini mbona mateka huyo amenyamaza. Masahaba wakasimulia walichofanya na Mtume s.a.w. akawambia hilo si sawa. Kama ni ujamaa humu pia wamo jamaa za masahaba zangu kadhaa, hivyo si adili kuwahurumia wengine na kutokuwajali wengine. Hapo akawaagiza waamue moja kati ya mawili ama wawalegezee kamba mateka wote au wamfunge mjomba wake kama walivyowafunga wengine. Bila shaka masahaba nao kwa kuangalia kisogo cha aliyewabeba wakaamua kuwalegezea kamba mateka wote na hapo Mtukufu Mtume s.a.w. akapumzika. Je uko mfano leo unaoweza kuoneshwa wa jinsi Mtukufu alivyowatendea kwa wema mateka wa vita?

Si hilo tu la mateka wa vita, lakini pamoja na kwamba maadui wa mtume s.a.w. ndio walioanzisha vita lakini kila alipokuwa akituma jeshi la kwenda kupambana na maadui kwa kuona mwenyewe hatokuwepo pamoja nao na hivyo kuna hofu ya kuchupa mipaka kila mara alimpatia mkuu wa msafara maagizo haya:

- Muda wote wadumu kwenye ukweli na kamwe wasiongope.
- Wasiiharibu miili ya watu watakaouwawa.
- Watoto na akinamama na vikongwe wasiuliwe.
- Watumishi wa dini walioamua kujifungia kwenye mahekalu yao wasiguswe.
- Waislamu watakapoingia ngome ya adui, wasifanye uharibifu, wasisababishe hofu kwa watu wa kawaida, wasizibe njia, wasikate miti, wasiharibu mazao, wasiharibu wala kuvunja nyumba za ibada au za huduma za jamii.
- Kwa kadri ya hali wamtie hasara ndogo adui na nafasi yoyote ya mapatano ya amani itakayopatikana wasiiwache kuitumia.
- Wafungwa wa kivita wasiteswe, wale walio ndugu wa karibu wawekwe sehemu moja na waislamu wajali zaidi shida za wafungwa wa kivita kuliko shida zao.
- Iwapo kwenye kundi la wafungwa wa kivita kutakuwa na waheshimiwa wao basi ni wajibu wa waislamu kuwaheshimu pia na mapungufu yoyote watakayofanya yasamehewe.
- Muislamu yeyote atakayemfanyia vibaya mfungwa wa kivita basi fidia yake ni mfungwa huyo kupewa uhuru wake.

Mtukufu Mtume s.a.w. alizisisitiza kanuni hizi kiasi hiki kwamba alisema yeyote atakayeshindwa kuziheshimu kanuni hizi atakuwa hapigani kwa ajili ya Mwenyezi Mungu bali kwa ajili yake mwenyewe na hatopata chochote zaidi ya hasara.

Tukio la suluhu ya Hudaibiya linatupa ushahidi mwingine juu ya sifa ya Mtukufu Mtume s.a.w. ya kupenda amani na watu wa dini zingine na kujali kuchunga ahadi. Kwa ujumla Mtume s.a.w. baada ya kupata agizo la kiungu na ahadi ya kimbingu kwamba ataingia mji wa Makka kwa amani alifunga safari yeye na masahaba zake 1500 kwa lengo la kwenda kuhiji. Lakini walipofika wakuu wa Makka wakawazuia kuingia. Baada ya majadiliano ya muda mrefu na pamoja na masahaba kung'ang'ania kwamba waingie Makka kwa nguvu na wanao uwezo wa kupambana na wakazi wa Makka. Mtukufu Mtume s.a.w. hakukubali mawazo yao, bali akakubali kuandikishiana

***Endelea uk. 5***

# Alivyowatendea kwa wema wasio Waislamu.

*Kutoka uk. 4*

mkataba wa amani na wakuu wa Makka, mkataba ambao kwa dhahiri ulionekana kana kwamba unawadhalilisha na kuwaonea waislamu lakini yeye hakujali hilo.
Kwenye uandishi wa mkataba huo na hata baadae kidogo kulitokea matukio yaliyothibithsa sifa za ajabu za Mtukufu Mtume s.a.w. za unyenyekevu, kupenda amani na kutimiza ahadi hata mbele ya maadui zake.
Katika uandishi wa mkataba waislamu walianza kuandika kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema mwingi wa ukarimu. Upande wa Makka ukiwakilishwa na kiongozi wao Suhail, ukakataa kwa madai kwamba hawamkubali Allah kuwa ni *Arrahmanir rahiim.* Mtume s.a.w. akasema sawa futa *Arrahmaanir rahiim* na bakisha *Bismillah* tu. Kisha ikaendelea kaundikwa huu ni mkataba baina ya Suhail ibn 'Amr, na Muhammad mtume wa Allah, lakini Suhail ibn 'Amr, akasema hakubali kuandika Muhammad Mtume wa Allah kwani yeye hamwamini kuwa hivyo bali iandikwe Muhammad bin Abdillah. Masahaba wakaonesha kukasirishwa kwao na kutishia kwamba hawakubali hilo na hivyo hakuna haja ya kuandikishiana mkataba wa fedheha kama huo. Lakini Mtume s.a.w. mwenyewe akasema nionesheni palipoandikwa *rasuulullah* na akapafuta.
Jambo lingine lilitokea kwenye tukio hilo la Hudaibiya ni kwamba katika mkataba iliandikwa kwamba mtu yeyote atakayekuja kutoka Makka kwenda Madina Mtume s.a.w. amfukuze. Lakini yule atakayekuja kutoka Madina kuja Makka makafiri wamzuie. Hapo hapo mara tu baada ya mkataba kusainiwa mtoto wa Suhail ibn 'Amr, akaja kwa Mtume s.a.w. akipiga magoti na akilia kwa uchungu na kumwambia kwamba yeye ameshaukubali Uislamu na anaendelea kuteswa na familia yake hivyo anaomba Mtume s.a.w. asimuache Makka bali aende naye Madina. Pamoja na huruma zote kwa waislamu wapya, Mtume s.a.w. akamwambia tayari ameingia mkataba na wakazi wa Makka na hakuna njia ispokuwa avumilie na abakie Makka kwa wakati huo akimuomba Mwenyezi Mungu amfungulie njia zingine.
Jambo lingine ambalo nalo lafaa kutajwa hapa ni hili kwamba waislamu walilalamika kwa nini tukubali mkataba huu unaotudhalilisha na kutunyima haki kwamba atakapokuja mtu kutoka kwetu kwenda kwa makafiri wa Makka wao wamzuie lakini atakayekuja kwetu akiwa amesilimu sisi tumrudishe? Kwa hekima ya ajabu Mtukufu Mtume s.a.w. akawaambia kwamba yule anayekuja kutoka kwao kuja kwetu tayari amekuwa muislamu na hivyo atakaporudi kwao atasaidia kuhubiri zaidi, lakini yule atakayetoka kwetu huyo tayari ameukana Uislamu sasa kuna haja gani ya kukaa na mtu aliyekwisha ukana uislamu? Ni bora tu ande mahala pengine. Kauli hii ya mtume s.a.w. pia inafuta wazo bovu la wale wadhanio kwamba eti wale waliooucha uislamu (walioritadi) hukumu yao ni kuuwawa. Kwani kama ingekuwa hivyo Mtukufu Mtume s.a.w. asingekubali waondoke bali angesema nao warejeshewe ili wahukumiwe kifo.

Tukio la ushindi wa Makka linaonesha kilele cha wema, uvumilivu, kusamehe kwa mtume s.a.w. kwa watu wa dini nyingine, bali maadui zake pia.
Akiingia mjini Makka na jeshi la watu 10,000 kwa ujumla ukiondoa tukio moja la mkazi wa Makka aliyeonesha upinzani kwenye pembe fulani ya mji, kwa ujumla damu haikumwaga na badala ya kulipiza kisasi Mtume s.a.w. akibubujikwa na machozi alitangaza kwamba hana cha kusema zaidi ya maneno ya ndugu yake Nabii Yusuf kwa ndugu zake kwamba:
... Hakuna lawama juu yenu leo; Allah Awasameheni, naye ni Mrehemevu zaidi kuliko wanaorehemu. (12:93).

Pamoja na kushiriki kwenye vita, Mtukufu Mtume s.a.w. kamwe hakukubali kwamba mali ya mtu asiyeshiriki kwenye vita ichukuliwe.

Tukio moja lilitokea kwenye vita ya Khibar. Mchungaji mmoja alisilimu na baada ya kusilimu akamueleza Mtukufu Mtume s.a.w. kwamba pamoja naye alikuwa na kundi la wanyama wa chifu mmoja wa Wayahudi ambao alikuwa na dhamana ya kuwarejesha kwa mwenyewe, je afanye nini kwani hawezi kurudi tena kwa watu baada ya kusilimu kwa ajili ya usalama wake? Mtukufu Mtume s.a.w. kamwe hakusema kwamba hii ni sehemu ya mateka bali alimwambia likusanye kundi la wanyama na kulisukuma kuelekea upande wa mji anaoishi mwenye wanyama wake bila shaka Mungu atawaongoza wafike kwa mwenyewe, na hilo ndilo lililofanyika na ikatokea hivyo.

Kwenye hotuba yake ya kuaga Mtukufu Mtume s.a.w. alitangza kwa ujumla kwamba tofauti yoyote, yoyote iwayo, ikiwemo tofauti ya kidini haimfanyi mtu kuwa bora kuliko mwingine au kuwa na haki ya kumdhulumu mwingine:
Sehemu ya hotuba hiyo ya kihistoria inasomeka:

Enyi watu, yale ninayoyasema mbele yenu yasiklizeni na myakumbuke. Waislamu wote ni ndugu - mmoja kwa mwenzake. Nyote ninyi ni sawa. Watu wote wako sawa, bila kujali taifa au kabila wanalotoka, au nafasi waliyonayo ya uongozi, wote ni sawa. Kama vile vidole vya mikono miwili vilivyo sawa ndivyo hivyo pia ***wanadamu walivyo sawa***, mmoja kwa mwingine. Hakuna mwenye haki ya kudai ubora wowote juu yamwingine. Yote ninyi ni ndugu.

Wasikilizaji wapendwa huyu ndiye Muhammad, aliye mbora wa Manabii, aliye na tabia njema kabisa, aliye rehema kwa walimwengu wote, Mwenyezi Mungu Amsalie yeye na ahli zake wote. Basi nasi tukiwa wafuasi wake wakweli tujitahidi kujipamba kwa tabia hizo njema ili tuioneshe dunia kwamba Islam sio dini ya fujo bali ni dini ya amani na kwamba kamwe haitoshinda kwa bunduki bali itashinda kwa hoja za wema zenye mantiki. Mwenyezi Mungu Atusaidie sana.

Waakhiru da'waana anilhamdulillahi Rabil'alamiin. Wassalaam alaikum warahmatullah wabarakaatuh.

# Al-Huda wachochezi, ipo haja ya kuwatazama kwa makini

**Imetayarishwa na Majls Ansar Sultanul Kalam Majlis Khuddamul Ahmadiyya – Tanzania.**

Ukiacha nukta tuliyomaliza kujibu hivi punde, dondoo nyingine aliyoandika mhariri huyu wa Al-Huda katika toleo lile la tarehe 17 – 23 Julai 2014, ilisomeka; 'Harakati za Ahmadiyya dhidi ya Uislam'. Na alipoona hatukujibu chochote katika toleo lake la tarehe 14 – 20 August 2014 sawa na mwezi Shawwal 1435 Hijria aliandika makala nyingine isemayo; 'Makadiyani waficha dawa za kulevya kwenye magunia ya mchele'.

Kabla ya kueleza chochote juu ya hiki alichoandika mhariri huyu wa gazeti la Al-Huda, tungependa kunukuu maneno ya Allah Aliyefundisha hivi; "Allah hapendi jambo baya lisemwe hadharani, ila kwa yule aliyedhulumiwa, na Allah ndiye Asikiaye, Aonaye" (Kurani 4:149).
Na katika kauli ya Mtume (saw) kuhusiana na mada hii aliwahi kusema; "Inamtosha mtu kuwa MUONGO aanze kuelezea kila analolisikia" (Sahihi Muslim).
Kama hiyo haitoshi sehemu nyingine anasema; "Imesimuliwa na Hadhrat Uqba bin Aamir (ra) ya kwamba; yeye alimuuliza Mtume (saw) ya kwamba uokovu ni nini? Akajibu uzuie ulimi wako, na nyumba yako ikutosheleze, na ulie juu ya makosa yako". (Tirmidhi).
Makala hizo mbili alizoziandika katika matoleo yake tuliyonukuu hapo juu AMEFTAFSIRI makala iliyoandikwa na mtu aliyejiita Dr. Said Rashid bila kuchuja kipi aandike kipi akiache, kwa kuwa wao ni mabingwa wa kunakili na kuandika (copy & paste). Waswahili wanaomsemo usemao; "Simba akikosa nyama hata majani hula". Ndivyo ilivyo kwa ndugu hawa, baada ya kukosa hoja katika itikadi za Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya sasa wameamua kuingia katika ukurasa mpya ambao ni wa hatari zaidi kwao. Naam! Sasa wameingia kwenye ukurasa wa 'MATUSI NA MASINGIZIO YA UONGO NA UCHOCHEZI'.
Kwani ukizitazama makala hizo ni za uzushi na hata yale yanayoonekana kufanana kwa mbali yamepitwa na wakati mno, kiasi cha anayesoma kushindwa kufahamu kiwango cha ufahamu wa mambo wa Mhariri huyu wa gazeti la AL-Huda. Kwani kwenye ile makala aliyoinakili na kuipa jina 'Harakati za Ahmadiyya dhidi ya Uislam', mwandishi wa makala ile aliandika habari nyingi za uzushi na uongo, lakini tutaziainisha chache ili hata mtu mwenye kiwango cha chini cha uelewa aone jinsi mhariri huyu alivyo na husuda iliyofikia kiwango cha kumpofusha macho. Aliandika;
- "Mirza Ghulam alizaliwa kati ya mwaka 1839 na mwaka 1840.
- Mirza alikuwa anakunywa pombe na dawa za kulevya.
- kwamba vitabu vyake havijatafsiriwa katika lugha ya Kiingereza ili kuuficha uwezo wake.
- Ya kwamba Mirza kaikataa JIHAD
- Kwamba kiongozi wa sasa wa Ahmadiyya anaitwa Mirza Tahir Ahmad n.k

Sasa tukijibu kwa ufupi mno tungependa kueleza kuwa, si kweli kwamba Mirza alizaliwa katika tarehe hizo alizozibuni yeye. Bali kwa faida yake tunamueleza kuwa Mujadid wetu wa karne ya kumi na nne (14) Mirza Ghulam Ahmad (as) amezaliwa tarehe 13 Februari, 1835 AD sawa na mwaka 1250 Hijria. Tazama haya katika vitabu vyote vya historia ya Jumuiyya hii kama; "Masihi Aliyeahidiwa" n.k ambavyo vinapatikana hapa Mnazi mmoja Dar es salaam ambapo ndugu wote mnakaribishwa kuja kujionea wenyewe ukweli huo. Au kama hamuwezi kufika tembeleeni website yetu yenye anuwani ya www.alislam.org au www.ahmadiyyatz.org (tafakarini maneno ya mtu huyu ambaye hata mwaka aliyozaliwa Mirza Ghulam Ahmad (as) haujui, je anaweza kusema nini dhidi yake kilichokuwa sahihi?
Hoja ya pili anasema (Mungu Apishe mbali) kuwa; 'Mirza Ghulam Ahmad alikuwa anakunywa pombe na dawa za kulevya'. Sasa ukiangalia maandiko ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) juu ya ulevi kwa kuwanasihi wafuasi wake anasema yafuatayo; "Dhambi ni sumu msiile, kumuasi Mungu ni kifo kibaya kiogopeni ….. mtu asiyetanguliza dini juu ya dunia kweli kweli hayumo katika jamaa yangu, mtu asiyeacha kitendo kibaya kama kunywa pombe, na kucheza kamari, na kutazama wanawake na kuzini na hiyana na rushwa na kila jambo lisilojuzu kutenda na asiyetubia kwa kweli, hayumo katika jamaa yangu". (Safina ya Nuhu uk.13).
Sasa je makatazo kama hayo yanaweza kutolewa na mtu ambaye mwenye anakunywa pombe? Acheni chuki ambazo hazina kichwa wala miguu. Mkishindwa hoja tu mnakimbilia matusi? Hayo sioyo matendo ya Kiislam!!.
Pia amedai kuwa vitabu vya Mirza Ghulam Ahmad havijatafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. HUO NI UONGO MKUBWA!!!. Kwani kuna vitabu lundo zima vya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ambavyo vimetafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. Mfano 'Philosophy of the teaching of Islam, Essence of Islam, Jesus in India, Ark of Noah' n.k kwa maelezo zaidi tembelea website iliyotajwa hapo juu ambayo ni www.alislam.org kisha tazama sehemu iliyoandikwa Library halafu ujisomee vitabu lukuki vya Hadhrat vya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) vilivyotafsiriwa katika lugha ya Kiingereza ili uongo uliounakili upate kuona mwanga!!!. (Kwani njia ya Muongo huwa ni fupi).
Pia amedai kuwa Mirza Ghulam Ahmad (as) amekataza JIHAD. Hebu tazameni maneno yake juu ya jihad halafu mtu apime mwenyewe je ni kweli Mirza Ghulam Ahmad (as) mekataza JIHAD? Anasema;
"Na kanuni ya pili ambayo nimeamrishwa juu yake ni kusahihisha maana isiyo sawa ya JIHAD inayojulikana baina ya Waislam wasiyo na elimu. Mwenyezi Mungu Amenifahamisha kwamba zile njia zinazofahamika siku hizi kuwa kuwa JIHAD ni kinyume kabisa na mafundisho ya Kurani Tukufu. Hakuna shaka ndani ya Kurani Tukufu mlikuwa na agizo la kupigana vita, ambalo lilikuwa lielewekalo zaidi akilini na lenye kupendeza zaidi kuliko lile la Yoshua mwana wa Nuni". Sasa kwa maneno hayo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) hajakataza

***Endelea uk. 6***

# Bustani ya Washairi

### AJABU YA PEPONI.....!

1 Editori wangu fundi, hodi hodi kwa ajenda
Nitue uga stendi, nina mada imetanda
Mdomo siweki gundi, ya peponi nimeganda
Ajabu pepo twapenda, ila kufa hatupendi!

2 Jambo kifo hatupendi, ajabu pepo twapenda
Na ajapolia bundi, jojto mwili na hupanda
Twavuka na Bara Hindi, matibabu kuyaunda
Ajabu pepo twapenda, ila kufa hatupendi!

3 Kamwe pepo hatuendi, sharti kifo kutenda
Katu mkato ushindi, njia zake panya kwenda
Kifo kipimo hadundi, cha uhai na huvunda
Ajabu pepo twapenda, ila kufa hatupendi!

4 Dhiki bure hazivundi, zina faraja matunda
Na methali siiundi, iko wazi bila funda
Uvumilivu kipindi, yahitajika kuwanda
Ajabu pepo twapenda, ila kufa hatupendi!

5 Meli kifo hawadandi, kwa hiari ni kupinda
Mashehe nao watendi, makasisi makamanda
Hata wajinyongao ndi, hujuta mithili punda
Ajabu pepo twapenda, ila kufa hatupendi!

6 Kifo usinipe lindi, niwaze zua vidonda
Kifo sirembe ja bendi, bali unipe kalenda
Mwili katu na sikondi, hima kuja nitadunda
Ajabu pepo twapenda, ila kufa hatupendi!

7 Muhoni mbali siendi, sifiki beti ya kenda
Nimetosha na sirandi, natulia mie kinda
Leo ni hai pa kundi, kesho kifo ni kiwanda
Ajabu pepo twapenda, ila kufa hatupendi!

"Poem Juggler"
Master JC Muhoni (Nguvu ya m2 mpya)
S.L.P 10960 MWANZA (0786 964992)

### USINGIZI

1. Usingizi nakuomba, muda sasa umefika
Macho yangu kuyafumba, nataka kupumzika
Niwe na wewe sambamba, hadi nitapoamka
Siwe mbali usingizi, njoo ninakuhitaji

2. Nipe njozi tamu tamu, usingizi natamka
Siyo zile za haramu, nikaja kuweweseka
Waja wakanilaumu, hata pia kunicheka
Siwe mbali usingizi, njoo ninakuhitaji

3. Niliwaze usingizi, watambua nimechoka
Uje bila pingamizi, name nipate kudeka
Kwako wewe nibarizi, na shuka kujifunika
Siwe mbali usingizi, njoo ninakuhitaji

4. Uniandame usiku, hadi na kupambazuka
Kero liwe marufuku, la sisi kutuzunguka
Nipate nyingi shauku, pindi nikigutuka
Siwe mbali usingizi, njoo ninakuhitaji

5. Mno ninakuhitaji, usingizi si dhihaka
Kwangu uwe ni mtaji, biashara nikitaka
Usiche kunifariji, mbele nikaadhirika
Siwe mbali usingizi, njoo ninakuhitaji

6. Tamati nimefikia, usingizi mshirika
Wito ukiusikia, hima ufanye haraka
Nyumbani kunijilia, karibu utapofika
Siwe mbali usingizi, njoo ninakuhitaji

7. Asubuhi niamkapo, nguvu tele mwilini
Umeondoka mchoko, akili zimejaa kichwani
Kazini nifikapo, kazi hainipi mtihani
Siwe mbali usingizi, njoo ninakuhitaji

*Al-Haj Abdallah Salim Seif Alhabsy*
*P.O.Box 1840 CODE 111,*
*Muscat Air Port, Seeb.*
*Sultanate of Oman*

### ELIMU

1. Kwa jina lake Mwenyezi, ninaimba kwa vituo,
Ninene na wanafunzi, masomo muhitimuo,
Nawaasa kwa mapenzi, shikeni hili zinduo,
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunai.

2. Elimu jambo azizi, ila inataka tuo,
Haitaki ubazazi, wa ngebe na matanuo,
Yataka uwe maizi, wa kukwepa michepuo
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

3. Elimu siyo hirizi, ya kufutikwa kwa nguo,
Bali ni kitu nyerezi, chataka msisimuo,
Sipoifanyia kazi, hutoka kwa mkupuo,
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

4. Elimu sio kitanzi cha kuuchosha mwilio,
Ni tunu ya kukuenzi, ndilo jema kimbilio,
Sifa ya Mola Mlezi, ifanyie piganio,
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

5. Elimu si kiumbizi, bali huleta tatuo,
Ni fani yenye uwazi, kwenye siri ni fichuo,
Huwezesha uchambuzi, kwa mambo ni fafanuo
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

6. Elimu ni tumbuizi, lilo chini ya ufuo,
Yataka uwe nyambizi, mzamiaji wa vyuo,
Vizuri ukiienzi, itakupa changanuo,
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

7. Elimu ni utambuzi, itafute kwa sumbuo,
Zamia yake mizizi, uombe na ufunuo,
Allah Aliye Mjuzi, atakujaza tambuo,
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

8. Elimu kwenye vizazi, inaleta mapinduo,
Jamii hupanda ngazi, ipate mwema mkuo,
Na huzalisha wajuzi, fani wazihukumuo,
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

9. Elimu ndio kurunzi, humulika machimbuo,
Huondoa vizuizi, na kukupa pambanuo,
Hata kwenye usingizi, hukufanyia situo,
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

10. Ni ashara beti hizi, hapa nifanye kituo,
Nawaasa wanafunzi, msiache mipekuo,
Kazaneni kuperuzi, kwa nguvu na makamio
Elimu ni ufunguo, wa akhera na dunia.

***Abdallah Khamis Mbanga (Kungwi)***
***Tambani, Mkoa wa Pwani***

### SHULE YETU

1. Allahu Mola Mjenga, Kwake tunatawakali,
Vijana tumejipanga, tunafanya mahafali,
Shule yetu ya Kitonga, hii mara ya awali,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

2. Shule yetu bado changa, ni haba kwa kila hali,
Mola Ishushie mwanga, iweze kufika mbali,
Wote wanaoinanga, kwa aibu wawe chali.
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

3. Shule yetu tunajenga, kwa pato letu kalili,
Kishida tunajikanga, japo tufike mahali,
Rabbi ondoa majanga, shule uipe sahali,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

4. Shule yetu imesonga, kwa maumivu makali,
Na hapa tulipogonga, twamshukuru Jalali,
Twaamini itanoga, ipigiwe na mithali,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

5. Shule yetu inalenga, kwenye ubora wa kweli,
Ingawa kuna visanga, hutokea kwa akali,
Tuna walimu vigaga, vilivyo huvikabili,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

6. Shule yetu huwakanga, wanafunzi madhalili,
Kitabia huwajenga, wakawa watu jamali,
Wanaozidisha nganga, kuwafuta haijali,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

7. Shule yetu inapinga, mambo yasiyo halali,
Matokeo ya kupanga, hatuyapi udalali,
Kibwebwe tunajifunga, tuzalishe vichwa nguli,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

8. Shule yetu tunaringa, haiongozi kufeli,
Bado iko kwenye anga, ya zilizo afadhali,
Ziro bado twazichenga, hazijapata mahali,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

9. Shule yetu hufinyanga, hata wakata boli,
Wataalamu wa chenga, wenye mashuti makali.
Wakenda Simba na Yanga, ni kikosi cha awali,
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

10. Shule yetu ninaaga, ni chuo cha maadili,
Uovu hauna swaga, na hatuupi kivuli,
Na chuya tutazipwaga, ziwe mchele wa kweli
Uidumishe Jalali, shule ya Ahmadiyya.

***Abdallah Khamis Mbanga (Kungwi)***
***Tambani, Mkoa wa Pwani***

### JUA LINATOA GIZA

1. Napita nakitafuta, kito hicho cha thamani
Jina lake sijapata, silijui asilani
Nakitafuta tafuta, palo wazi na pembeni
Jua linatoa giza, mwanga tutatoa wapi?

2. Sielewi pa kupita, hamadi we! Kibindoni
Ni vipi nitakiita, kije haraka nyumbani
Ngoma gani takung'uka, upesi kije ngomani?
Jua linatoa giza, mwanga tutatoa wapi?

3. Nasikia kinameta, jakawarira juani
Kwa shani chametameta, kama nyota maangani
Lini nitakifumbata, nikivae jakidani?
Jua linatoa giza, mwanga tutatoa wapi?

4. Kupumzika nasita, sitatua abadani
Iwe shari na matata, nitapita msituni
Chochote nitachokuta, nitakitoa njiani
Jua linatoa giza, mwanga tutatoa wapi?

5. Tamati bwana pulata, mahiri wa kiyunani
Pango limevaa tata, viumbe tumo gizani
Taratibu tunanyata, kutoka humo pangoni
Jua linatoa giza, mwanga tutatoa wapi?

***Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)***
***Kiwalani Migombani – Dar es salaam***

# Al-Huda wachochezi

***Kutoka uk. 5***

jihad, bali amekataza maana au tafsiri mbaya ya neno Jihad inayoeleweka leo hii, makundi kama ALQAIDA, TALIBAN, SELEKA, BOKO HARAM, AL-SHABAB N.K wanachokifanya siyo jihad bali ni dhuluma kwa watu wasio na ni hatia na ni makosa kuziita harakati hizi za kisia kuwa ni Jihad.

Akiwaelekea wafuasi wake kuwaongoza kwenye jihadi ya kweli na maana ya kweli ya Jihad, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) anawahimiza:

Katika wakati huu kimahususi naielekeza Jumuiya yangu wanaonikubali kuwa ni Masihi Aliyeahidiwa, kwamba daima wakae mbali na tabia hizi chafu. Mungu amenituma kuwa Masihi na amenivika vazi la Masihi a.s. Mwana wa Mariamu.

Kwa hiyo ninawausieni; epukaneni na uovu na muwe na huruma ya kweli kwa wanadamu. Safisheni nyoyo zenu dhidi ya chuki na kinyongo, kwa maana kwa kushika tabia hii mtakuja kuwa kama malaika. Ni chafu na haifai dini ile ambayo inakosa huruma kwa wanadamu, na imechafuka njia ile iliyojaa kisirani kwa msingi wa tamaa za kibinafsi … kuweni na huruma kwa wote kwa ajili ya Mungu ili kwamba muweze kuonyeshwa ukarimu kutoka mbinguni. Njooni na nitakufundisheni njia ambayo itafanya nuru yenu ing'ae juu ya nuru zote. Acheni bughudha zote na uovu na wahurumieni watu na jitupeni kwa Mungu ...

.. Nimekuja kwenu na amri: Jihadi kwa panga kuanzia wakati huu na kuendelea imekwisha, Jihadi ya kuzitakasa roho zenu lazima iendelee. Sisemi haya kwa utashi wangu. Kwa hakika huu ni utashi wa Mungu.

Tafakarini hadithi iliyomo katika Bukhari ambamo imesemwa kwamba Masihi Aliyeahidiwa ataondosha kupigana kwa ajili ya imani. Sawa na hilo ninawaamuru wale waliojiunga na kundi langu kwamba waziache fikra kama hizo. Wazitakase nyoyo zao na kukuza ukarimu wao na wanapaswa wawahurumie wenye shida. Waeneze amani duniani kwa kuwa kwa kufanya hivyo wataifanya dini yao ienee pia.

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Kazema amjibu Bishazo

## Sehemu ya Mwisho

### Kutoka toleo lililopita

Nukuu ya Yesu mwenyewe.
***(yohana 3:13) Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni yaani mwana wa adamu.***

Tazama kama nilivyoandika katika makala yangu uliyojaribu kujibu, bwana Bishazo, naamini ni kweli nukuu ile hukuipenda, lakini ndio ukweli. Hapa Nabii Issa a.s anataka kuwafikirisha au kutufikirisha:- Hebu tutafakari kushuka kwake kulikuwa kwa namna gani? Si alizaliwa kwa uchungu na kukuwa kama kawaida ya tulivyoshuka mimi na wewe na kama hivyo kupaa kwetu kutakuja kuwa kama alivyopaa yeye kwa Umauti wa kawaida, na ndivyo tulivyoshuhudishwa ukweli huu na Hatamu wa Manabii Muhammad Mustafaa s.a.w.
Mtukufu Mtume wetu S.A.W pamoja na masahaba wake walielewa bila shaka yeyote kuwa Issa bin Mariam alikwisha fariki. Malaika Jibril alimfahamisha Mtume s.a.w kuwa yeye Mtume ataishi nusu ya umri wa Mtume

aliyemtangulia. Kwa maana hiyo basi na kutokana na hadithi katika vitabu vya Kanzul Ummal jal. 6 uk. 160 na pia Hujajul Karamah uk. 428 Nabii Issa a.s aliishi miaka 120. Katika muda huo aliweza kuwafikia Wanaizraeli wote wale Makabila 10 yaliyoishi huko na pia katika madhehebu yao 72 aliyoyakuta zama hizo na kuwafikishia na kuwafundisha aliyotumwa nayo kutoka kwa Subhana Wataallah.
Alifariki akiwa amekamilisha kazi yake katika mji wa Srinagar Kashmir na kaburi lake lipo huko. Wanahistoria na Wanasayansi wamejiridhisha juu ya hilo na hata BBC wamekwisha tengeneza documentery juu ya swalla hili. Yesu alikuwa ni miongoni mwa Mitume waliopandishwa daraja, na neno BAL RAFAAHUL LAAHU ILAIHI ni kupandishwa daraja na wala si kubebwa kupelekwa kwa Mungu Mwenyezi **kihalisia** na kiwiliwili kile cha udongo.
***Kur 2:254 Hao Mitume Tumewafadhili baadhi yao zaidi kuliko wengine miongoni mwao wako ambao Mwenyezi Mungu Alisema nao wengine wao Akawapandisha daraja na Issa mwana wa Mariamu tukampa Ishara zilizo wazi na tukamsaidia kwa Roho takatifu …***
Wakati wa Nabii Issa bin Mariam walikuwepio Manabii wawili yeye na Nabii Yahaya . hapa usaidizi wa Roho Mtakatifu (Malaika Jibril) ndizo package ndani ya neno bal rafaahul Laahu Ilaihi, bila kusahau kwamba walipita Manabii wengi baada ya Musa a.s lakini Yeye ndiye aliyeteuliwa kuisadikisha Taurati.
Mtume Mtukufu Muhamadi s.a.w pia alishushwa Maka kwa maana nyingine ya kwamba ataufikia mji huo na kuukalia. Maneno ***kushuka kupandisha kuteremsha*** haya yanapotumika wakati wote huwa na maana tu ya kimajazi au kiistilahi ***kur 90:3***
***Nawe utashuka katika mji huu.***
Nitaanza kumnukuu Mathayo mtakatifu fungu lake la 28:11 hadi 28:16 neno kwa neno ambapo utaona kuwa uvumi ulivumishwa na ili kuusimika barabara ilitumika Hongo, kwa kuwa kulikuwa na maslahi kwenye pande zote na uvumi ule umeshika baina ya watu mpaka hii leo. Biblia inathibitisha hivyo. Ni vizuri wewe msomaji na Bishazo usome na uelewe hakika ya mambo. Sasa kwa kuwa hawa wawili hawakumwona Yesu akipaa, nani mwingine alimwona Nabii Issa a.s Akipaa? Bishazo upo hapo? Kwa

maana hiyo Hakuna aliyepaa mbinguni hapa pia Uzeil na Elisha (Eliya) pia hawakupaa mbinguni, walitoweka na kufia mahali ambapo watu wao hawakuweza kupabaini.
Sasa basi anza kusoma nukuu za Watakatifu hao na makala itaishia hapo, ila kama mheshimiwa Bishazo moyo wako, kwa masikitiko makuu na hasara, utakuwa bado haujapata yakini na kwamba imani yako hujaiona kwamba inamdhalilisha Allah S.W (Ee Allah tusamehe) kwamba Alishindwa na Wayahudi wale na kumkimbiza Nabii wake kwa njia za woga kabisa na kuvunja kawaida Alizokwisha ziwekea misimamo. Na siku ya kiyama Allah S.W Atamlamu nani Ikiwa Ataacha Wayahudi waamini Issa a.s amefia msalabani kwa hiyo si Nabii mkweli.
Paulo aliyemfuata kumtafuta Yesu KWA SHARI na kukutana naye Damascus kisha akabadilika na kuwa mfuasi wake ambae ndiye hasa aliyekuja kuutengeneza Ukristo huu wa leo kinyume na maagizo ya Yesu kwa Petro na wanafunzi wake, inatutambulisha kwamba Wayahudi walitambua hawakufanikiwa hila yao na hivyo hawawezi kukwepa dhambi ya jaribio lile na dhambi ya kutomwamini mpaka kiyama.

*MATHAYO MTAKATIFU*
*28:11-15 Nao wale walipokuwa wakienda tazama baadhi ya askari waliingia mjini wakawapasha wakuu wa makuhani habari ya mambo yote yaliyotendekea. Wakakusanyika pamoja na wazee, wakafanya shauri, wakawapa askari fedha nyingi. Wakisema semeni ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku, wakamuiba sisi tulipokuwa tumelala. Na neno hili likisikilikana wa liwali, sisi tutasema naye, ninyi tutawaondolea wasiwasi. Basi wakazitwaa zile fedha, wakafanya kama walivyofundishwa. Na neno hili likanea kati ya Wayahudi hata leo.*
*28.16 – 20 Wale wanafunzi kumi na mmoja wakenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu. Nao -walipomwona, walimsujudia, lakini baadhi yao waliona shaka. Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba Na Mwana Na Roho Mtakatifu na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*
Mwanafunzi wa pili aliyekuwa nae Yesu mpaka dakika ya mwisho ndiye Yohana Mtakatifu ambaye anazieleza hivi hizo dakika za mwisho.

*21:17 Akamwambia mara ya tatu, Simon wa Yohana, wananipenda? Petro alihuzunika kwa vile alivyoambiwa mara ya tatu wanipenda? Akamwambia, Bwana, wewe wajua yote; wewe umetambua ya kuwa nakupenda. Yesu akamwambia, lisha kondoo zangu.*
*21:18- 23 Akasema Amini, Amini nakuambia, wakati ulipokuwa kijana, ulikuwa ukijifunga mwenyewe na kwenda utakako, lakini utakapokuwa mzee, utainyoosha mikono yako, na mwingine atakufunga na kukuchukua usikotaka. Akasema neno hilo kwa kuonyesha ni kwa mauti gani atakayomtukuza Mungu. Naye akiisha kusema hayo, akamwambia. Nifuate. Petro akageuka akamwona yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu anafuata, (ndiye huyo aliyeegama kifuani pake wakati wa kula chakula jioni, akasema, Bwana, ni nani akusalitiye?) Basi Yesu akamwona huyo akamwambia ikiwa nataka huyu akae hata nijapo, imekupasaje wewe? Wewe unifuate mimi. 23 Basi neno hilo lilienea katikati ya ndugu ya kwamba mwanafunzi yule hafi. Walakini Yesu hakumwambia ya kwamba hafi; bali ikiwa nataka huyu akae hata nijapo imekupasaje wewe 24 Huyu ndiye yule mwanafunzi ayashuhudiaye haya, na aliyeandika haya nasi twajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli.*

Katika nukuu hizo kuna mambo muhimu ya kuzingatia, Paulo anatabiriwa hapo kuja kumpeleka Simon wa Petro kuwahubiria na kupeleka dini sehemu nyingine asikokutaka

kinyume na maelekezo ya Nabii Issa a.s Mwenyewe.
***Mathayo 15:26 Si vyema chakula cha watoto kuwatupia mbwa.***
***Mathayo 15:24 Sikutumwa ila kwa kondoo walipotea wa nyumba ya Israel.***

Sasa Bishazo naomba nimalizie na Aya mbili tatu zifuatazo:-
***Kur. 7:25- 26 Akasema Nendeni, ninyi kwa ninyi m- maadui, Na kao lenu litakuwa katika ardhi na posho kwa muda Akasema mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo.***
Leo kuna mwanadamu anaishi mbinguni. Mpaka tujesema Nabii Issa aliishi duniani basi Bishazo akirudi Isaa a.s, na aje aishi miaka 5000 lau sivyo kwa kipimo chochote miaka 45 kwa 2000 huyo si wa Aya hiyo hapo juu. Je umefika? Je (Mungu apishe mbali) kuna haja ya kuletewa wanadamu Ayah hii.
***Kur: 50:30***
***Kwangu kauli haibadilishwi wala mimi siwadhulumu watumishi.***
Ndugu yangu Bishazo mimi naishia hapo. Si vyema wewe kushika nukuu za wapinzani wa Mitume na bila kufanya utafiti ukazitumia, Mwenyezi Mungu atakuchukia utakapozidi. Mtume mwongo dini yake haitoki hata nje ya mji wake na huuwawa. Ikiwa Mtume Mtukufu angezua baadhi ya maneno kuwa yametoka kwa Mwenyezi Mungu, Allah Angemkatisha Utume wake. Nae aliishi miaka 23 katika Utume wake. Seyyidna Ahmad aliishi miaka 26 katika Utume wake. Mtume mwongo

HAFAULU Ahmadiyya sasa inateka Misikiti hata hapa Tanzania na Makanisa Ulaya.

Wabillah Toufiq
Eng K.S. Kazema
MOROGORO

Wabillah Toufiq
Eng. Kaya S. Kazema
Morogoro

## IJTIMAA YA ANSARULLAH 2014

**Tumo kwenye mwezi Novemba sasa, mwezi ujao ni Desemba. Mwezi Desemba katikati, yaani tarehe 13 na 14, 2014, Tanzim ya Majlis Answarullah Tanzania kama kawaida itafanya Ijtimaa na Shura. Shughuli hizi zitateendeka kule Kitonga Inshallah. Siku zimekaribia mno, tuwe tayari kuhudhuria Ijtimaa hii bila kukosa. Sadri sahib, muadham Inayatullah S. Nakuchima anategemea kwamba kila Answarullah ametimiza wajibu wake wa kutoa michango yake yote na sasa anasubiri muda tu wa kufika kwenye viwanja vya shughuli zetu. Wajumbe wote wa Ijtimaa na shura wanategemewa kuwapo kwenye viwanja na ukumbi wa mikutano yetu kule Kitonga kuanzia tarehe 12 Desemba 2014, Mwenyezi Mungu Amfikishe hapa kila mjumbe salama usalimini. Pamoja na hayo, Sadri sahib anamkaribisha kila mtu anayependa kusikia, kuona na kushuhudia ukweli wa Seyidna Ahmad (as) wale walio karibu na pale tunapofanyia shughuli zetu tunawakaribisha sana. Tafadhali karibuni nyote.**

# Nafasi ya Qur'ani tukufu katika maisha ya kila siku ya mwaminio.

*Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2014 na Mwl. Shamuni Juma*



*Mwl. Shamuni Mwishehe Juma akiwasilisha hotuba yake wakati wa Jalsa Salana ya 45 iliyofanyika Kitonga Dar es Salaam*

KURANI TUKUFU NI NINI

Qurani tukufu ni kitabu chanye sheria iliyokamilika kutoka Kwa Allah Kwa ajili ya kumuongoza mwanadamu. Ni kitabu kilicho kamilika chenye sheria, kanuni na taratibu zote zinazofaa mwanadamu wakati wote mpaka kiyama.

Kurani tukufu inaweza kumnyanyua mwanadamu na kumfikisha mpaka daraja la juu kabisa kiroho na hata kiustaarabu, Na kwa muujibu maelezo ya Masihi Aliyeahidiwa a.s Qurani tukufu inaweza kumfikisha mtu (mwenye kuifuata kikamikifu) mpaka daraja la Unabii. Ni kitabu pekee kilichoahidiwa kupewa ulinzi kamili na Mwenyezi Mungu, na kisichoweza kufikiwa na batili mbele yake na nyuma yake. Mwanadamu hata aendelee vipi katika elimu ya Sayansi, teknolojia n.k lakini kamwe hataweza kukosoa hata fundisho moja la kurani tukufu.

Qurani tukufu imetoa mchango mkubwa sana katika ustawi na maendeleo ya dunia na yakwamba wanadamu muda wote wanaendelea kufaidi neema na fadhila nyingi kwa kuwepo kitabu hiki kitukufu.

Mwalimu mkuu wa kufundisha Kurani tukufu zama hizi yaani - Masih aliyeahidiwa a.s amepata kusema kuwa :- "Kheri na baraka zote zinapatikana katika kurani tukufu"

Tena amesema Mau'uud a.s kuwa :- "Kurani tukufu ni njia iliyonyooka kuliko njia zingine zote. Ni njia iliyojaa nuru zenye mtiririko wa yakini, ni Kiongozi kamili inayojitosheleza kusuluhisha na kuamua magomvi yote ya kidini (na hata ya kawaida) Kila aya na kila neno lina maelfu ya mtiririko inayojitosheleza na iliyojaa maji ya uzima kwa ajili yetu na ina johari ya yakuti nyingi ndani yake zinazodhihirika kila siku. Hii ndio miski nzuri tunayoweza kupimia tofauti baina ya uongofu na upotovu. (TZAALAE AUHAAM RUHAANI KHAZAIN JAL. 3 UK 381)

Akitoa maelezo zaidi juu ya Qurani tukufu Masihi mauud a.s anasema, "Elimu zote zimo ndani ya kurani tukufu ila watu tu wanashindwa kuzielewa"

Tena anasema Hadhrat Ahmad a.s kwamba " Kila elimu imo ndani ya Kurani tukufu, lakini watu wameelekea katika moshi unaoangamiza"

Akaendelea hadhrat Masih mau'ud a.s anasema :-

"Uzuri wa kurani tukufu, hii ndio nuru ya kila mwislamu, wengine wanausifu mwezi na sisi wetu, Tumeangaza kila mahali, lakini mfano wake hupatikani, kwani huu tu ndio ufunuo wake Mwenyezi Mungu"

Kitika moja ya mashairi yake, Hadhrat Ahmad a.s alisema:- "Ee mola mtukufu, Qurani yako ndio dunia ya ajabu, na yote ya muhimu yamo ndani. Tumetembea dunia nzima, maduka yote tumeyachambua lakini kinyaji halisi cha elimu na maarifa tumekipata humu humu"

Kwa kauli fupi na nzito hadhrat masih aliyeahidiwa a.s alisema :- "Kutengana na kurani tukufu hata kidogo ni maangamio yetu"

HAJA YA KURANI TUKUFU,PAMOJA NA KUWEPO VITABU VINGINE

Hili ndilo Swali ambalo huleta shida katika akili za wanadamu, kwamba wakati Veda, Taurati, Injili na Zaburi vilikuwepo duniani, kulikuwa na haja gani basi ya Mwenyezi Mungu kuleta kitabu kingine - Qurani tukufu.

Majibu yanaweza kuwa mengi na kwa njia mbalimbali.

Lakini kwa kifupi Mwenyezi Mungu anasema :- "Na kwa yakini tulimpa Mussa kitabu, lakini zikatiwa hitilafu ndani yake". (11:111)

Ni ukweli usiopingika kwamba kutokana na misukosuko mingi na mikubwa waliopitia wana wa Israel, hivyo ilikuwa vigumu kwao kuvilinda vitabu vyao,Swali lingine linazuka hapa, nalo ni hili kuwa wana wa Israel walishindwa kuvilinda vitabu vyao je? Mwenyezi Mungu nae alishindwaje kufanya kazi hiyo?

Jawabu lake ni hili kwamba Sheria na kanuni za vitabu hivyo hazikukusudiwa kuwaongoza binadamu wote ulimwenguni na wala hazikukusudiwa kudumu mpaka siku ya kiyama. Bali sheria hizo zilikusudiwa kufanya kazi katika mazingira maalumu na watu wa nyakati maalumu

Mfano Tuangalie kama sheria yaa kisasi iliyomo katika Agano la kale haiwezi kufaa katika zama za ustaarabu na sheria ya kusamehe kupita kiasi iliyomo katika injili haiwezi kufaa katika zama zilizoshamiri uhalifu

Hii ndio sababu katika vitabu hivyo Mungu amesemwa kuwa ni wa Israel, na nabii Issa a.s alikuja (alitumwa) kwa waisrael, siku ya kiyama hukumu ya wema na wabaya itawahusu Kabila 12 za wana wa israel

Hivyo baada baada ya sheria hizo kufanya Kazi katika zama husika na kushindwa kukidhi mahitaji wakati huu.(Ndipo Mwenyezi Mungu akatufanyia ihsani kubwa kutuletea kitabu hiki - kurani tukufu iliyojaa kila aina ya uzuri, elimu, hekima n.k)

Zaidi ya hayo, tunaelezwa kuwa Agano jipya lilipatikana kwa kupiga kura ya ndio au hapana, hii ni baada ya kuwepo vitabu vingi sehemu mbali mbali ndipo katika mwaka wa 350 AD uliitishwa mkutano mkubwa na vitabu vikaletwa na ili kuamua ni vitabu gani viitwe neno la Mungu ikabidi ipigwe kura ya ndio au hapana. Vile vitabu vilivyopata hapana nyingi vikakataliwa na kutupwa na vile vilivyopata ndio nyingi vikapitishwa kuwa neno la Mungu.

Hivyo imani ya Mkristo mmoja ilitegemea kura ya mkristo mwingine, Lakini mbaya zaidi ni kuwa wakati kura hiyo inapigwa imani ya kipagani ilikuwa imekwisha ingia na kushamiri katika ukristo. Ndio kusema kuwa kura nyingi za ndio zilikwenda kwenye vile vitabu vinavyokubaliana sana na itikadi mpya.

Katika kitabu cha Mabaniani kiitwacho MANU SMRITI imeandikwa hivi:- "Endapo Brahmin (Baniani Sharif) hataweza kumlipa mmoja wa mabaniani koko deni lake basi mdai huyo hana haki ya kudai mali yake. Lakini endapo mmoja wa mabaniani koko atashindwa kurudisha mali aliyokopeshwa na baniani sharifu, basi ni sharti afanywe mpagazi wa huyo mdai wake hadi pale atakapoweza kulipa mkopo huo wote" (10:35)

Haya ndio tuyasomayo kutoka katika vitabu vilivyopita, kana kwamba Mungu wa vitabu hivyo hata hakujali kabisa thamani ya utu na ubinadamu.

Hii ndio sababu ya mahitaji yasiyokwepeka ya kupata kitabu maalum kutoka kwa Allah kitakacho ondolea mbali karaha na jefule hizo zote.

Na kitabu hicho si kingine ispokuwa ni Qurani tukufu ambayo ndani yake mna kila fundisho lililo hai na la kumfaa mwanadamu wakati wote. Kwa mfano Kurani tukufu inasema :-

"Hakika Mwenyezi Mungu anawaamuruni ya kwamba mrudishe amana kwa wanaozistahili, na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu" (4:59)

Katika aya hii Mwenyezi Mungu ameeleza msingi muhimu sana katika ngazi zote kuanzia viongozi hadi kwa raia wa kawaida na kwamba uadilifu utendeke na kila anyestahili apate haki yake bila kusumbuliwa au kuonewa.

Tena Kurani tukufu inasema:- " Enyi mlioamini kuweni imara katika kusimamia uadilifu mkiwa mashahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hata kama ni dhidi yenu wenyewe au wazazi (wenu) na jamaa wa karibu. Awe tajiri au maskini,Menyezi Mungu yu karibu nao zaidi wote wawili" .....(4:136) kwa muujibu wa aya hii, ushahidi wa kweli hapana budi utolewe bila ya kujali ushahidi huo utamnufaisha nani au utamdhuru nani. Na bila ya kuangalia utajiri wa mtu, cheo, au heshima yake.

Naye mtume s.a.w alisema hata kama ni Fatuma r.a akiiba atakatwa mkono.

Ni sikitiko kubwa kwamba leo hii fundisho hili zuri limepewa kisogo na walimwengu na matokeo yake ni machafuko yasiyoisha sehemu mbali mbali duniani.

Tena kurani tukufu inasema :- " Na uadui wa watu usiwashawishi ya kwamba msifanye uadilifu. Shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa." (5:9) Hakika hakuna kitabu kingine kinachotoa mafundisho mazuri juu ya haki na uadilifu kama haya. Mfuasi wa kweli wa Kurani tukufu anatakiwa awatendee haki si tu Waislamu bali pia wasiokuwa waislamu na hata maadui zake.

Tena kutani tukufu inasema :- " Msidhulumu wala sidhulumiwe" (2:280), kwa hakika huu ndio mzizi muhimu na roho ya amani na usawa, haki na uadilifu. Yani kama vile ambavyo mtu yeyote hapendi kuonewa, kubugudhiwa na kudhulumiwa, hivyo ndivyo anatakiwa naye asiwatendee wengine.

Akifafanua hili Mtume (s.a.w) amesema :-

"Naapa kwa yule ambaye uhai wangu upo mikononi mwake, hataamini yeyote miongoni mwenu mpaka ampendelee nduguye kama vile anavyojipendelea nafsi yake" (BUKHAR/MUSLIM)

NI VIPI MWAMINIO ANATAKIWA AIANGALIE, AISHUGHULIKIE, AISOME NA KUIFUATA QURAN TUKUFU KATIKA MAISHA YAKE YA KILA SIKU.

Mwenyezi Mungu anasema

"Basi ni hadithi gani watakayoiamini baada ya Mwenyei Mungu na aya zake". (45:7) Kwa mujibu wa aya hii mwislam anatakiwa kuiheshimu na kuitanguliza Kurani tukufu juu ya Hadithi au kitabu kingine chochote kile kiwacho. Hii ni kwa sababu Kurani tukufu imekusanya kila fundisho lenye kumfaa binadamu. Na kurani tukufu inasema :-

"Na ziko kwake funguo za ghaibu hakuna azijuaye ila yeye tu, na anajua yaliyomo barani na baharini na halianguki jani ila analijua, wala punje katika giza la ardhi wala kilichorutubika,

*Endelea uk. 9*

# Nafasi ya Qur'ani tukufu

*Kutoka uk. 8*

wala kilichoyabisika, ila yamo katika kitabu kibainishacho" (6:60).

Ni wazi kuwa katika aya hii Mwenyezi Mungu anabainisha ujuzi wake uliomkamilifu na ya kwamba hakuna chochote kinachotokea au kutendeka isipokuwa Kurani imekwishaeleza habari zake mapema kabla, Tena Kurani tukufu inasema :-

"Na bila shaka tumewaeleza watu namna kwa namna katika Qurani hii kila mfano" .(18:55).

Hapa Qur'aani inabainisha wazi kuwa, Mwenyezi Mungu ametumia kila aina ya njia ifaayao katika kumwelekeza, kumfundisha na kumuongoza mwanadamu. Na ni hakika kuwa tunapoitwalii Qurani tukufu tunaona kila aina ya mifano, maonyo na kadhalika. Hii yote ni katika kumrekebisha na kumwongoza mja wake. Hivyo kuna kila sababu ya kujifunza, kusoma na kuifanyia kazi Qurani tukufu zaidi ya hayo Quran tukufu inasema:-

"Wape habari njema watumishi wangu, ambao husikiliza kauli ( Qurani) kisha wanafuata wema wake" 39:18-19.

Hapa kuisoma Qurani tukufu, kuisikiliza na kufuata mafundisho yake. Kumehimizwa na sababu yake

I wazi kama ilivyoelezwa hapo na katika aya hii ifuatayo:-

"Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu ambaye amemteremshia mtumishi wake kitabu, na hakufanyia wala hakukifanyia tenge" (18:3) Katika aya hii Qurani tukufu imejieleza kwa ufasaha ya kwamba ni kitabu kilichotimilifu na kisicho kasoro wala dosari yoyote ndani yake - na jambo hili limethibitishwa pia na wataalamu na wasomi ulaya Magharibi

Tena Qurani tukufu inatueleza kuwa:-

"Na haiwezekani Qurani hii kutungwa na yeyote ispokuwa Mwenyezi Mungu, Basi inyosadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya kitabu. Haina shaka, imetoka kwa Mola wa Walimwengu" .. (10:38)

Aya hii inatupa habari kuwa Qurani si kazi ya mikono ya mwanadamu yeyote aliyetokea katika dunia hii, bali ni uteremsho wa yule aliye ni mjuzi na mkamilifu pekee - yaani Allah

Zaidi ya hayo Qurani tukufu yatupasha habari kuwa:-

"Enyi watu: hakika yamewafikieni mawaidha kutoka kwa mola wenu na ni tiba ya yale yaliyomo vifuani, na ni mwongozo na rehema kwa waaminio". (10:58)

Katika aya hii Qurani yatueleza kuwa yenyewe ni ponyo - yani tiba ya maradhi yote ya roho. Takitwalii vizuri taarikh ya islam tutagundua ukweli wa jambo hili. Qurani imewainua waarabu kutoka katika ulevi wa kutwa mara tano na wakawa watu wakufanya ibada kutwa mara tano. Wakaacha kuabudu nyota, mawe na masanamu na wakajua thamani ya kumwabudu Mwenyezi Mungu. Na wakaacha kucheza kamari na wakatambua kwa njia pekee ya kujiongezea mali ni kufanya biashara pamoja na Mwenyezi mungu yaani kutoa katika njia ya Allah kama vile hawakuwa na akili timamu.

Matokeo yake ni kwamba vizazi vyao vinafaidika hadi leo. Wakaacha magomvi na vita visivyo na maana wakawa laini kama maji - Ingawa katika njia ya Allah walikuwa wakali na mastadi sana.

Wakaacha kuuwa watoto wa kike na wakafahamu thamani na umuhimu wa uhai wake. Wakaacha ujahili na wakatambua umuhimu na thamani ya elimu. Wakaacha shirki na kumtegemea Allah - Haya yote ni matokeo ya mafundisho mazuri ya Qurani tukufu

Kama tuitadabbur vizuri Qurani tukufu tutagundua kuwa sio tu ni tiba ya maradhi ya kiroho, bali pia ni twiba hata kwa maradhi ya mwili pia. Aya zake za mwanzo tu zinaonekana kushughulikia zaidi masuala ya afya ya mwili.

Hii inathibitika zaidi pale inaposema: yaani`soma ` Hapa suala la elimu ambayo ndio msingi mkuu wa kila kitu,limehimizwa- Na leo hii jambo hili liko wazi zaidi, kwani hatuwezi kupata waatalam wa fani mbalimbali ikiwemo afya bila elimu. Leo hii tunaelezwa kuwa magonjwa mengi yanayo tukabili yana yanasababishwa na ulaji wa ovyo. Kuhusu hili qurani tukufu inatufundisha kuwa:- "Enyi wanadamu'shikeni mapambo yenu wakati wa kila sala,na kuleni na kunyweni wala msipite kiasi"(7:32) katika aya hii, kwamza tumeelezwa suala zima la usafi na kisha ndipo Mwenyezi Mungu anatueleza utaratibu mzima wa ulaji wa chakula, kwamba chakula ni lazima kiandaliwe sawa na mahitaji halisi. Maswahaba wa Mtume s.a.w walizingatia vizuri sana fundiso hili.

Inasimulia kuwa alifika mganga fulani Madina wa kwanza kutibu watu. Alitoa huduma hiyo kwa miaka mingi, la ajabu ni kuwa katika wateja wake waislamu hawakuwemo. Jambo hili lilimtatiza sana na akataka kujua ni siri gani waliyonayo waislamu kiasi ambacho hawaendi kwake kupata matibabu. Akaenda kwa Mtume mtukufu (s.a.w) ili kumuuliza juu ya jambo hili. Alimkuta mtume (s.a.w) akiwa amekaa na maswahaba wake kadhaa. Akajitambulisha kuwa yeye ni mganga na yupo hapo Madina kwa miaka kadhaa, jambo linalomstaajabisha ni kuwa miongoni mwa wateja wake, hawaoni waislamu kwenda kupata huduma kwake. Katika jibu lake fupi lililokuwa na maana pana sana, Mtume mtukufu (s.a.w) alisema:- Yaani " Sisi ni watu ambao hatuli mpaka tupate njaa"

Hii inamaana kuwa mtu (watu) anatakiwa kula pale anaposkia njaa na kuacha pale njaa ituliapo. Na chakula kinatakiwa kiwe halali na kisafi - 2:169

Waila kula kusikokuwa na mpangilio, husababisha mlundikano wa sumu mwili na hivyo kuleta matatizo mengi zaidi ya hayo.

Qurani tukufu imetufundisha na kutuwekea ibada ya saumu kwa utaratibu mzuri sana na Mtume (s.a.w) alisema fungeni mpate afya.

Na kwa muujibu wa utafiti wa wataalamu wa afya wanasema kwa Swaumu ndio kinga namba moja dhidi ya maradhi.

Kwa ufupi ni kuwa Qurani tukufu imetufundisha mambo mengi bali yote yanayotufaa katika maisha yetu ya kila siku kama vile mikataba ya kimataifa 2:83

Muda wa miaka 2 ya kunyonyesha watoto 2:243

Mirathi Sura ANNISAA kusuluhisha wanandoa 4:36 na kusuluhisha migogoro ya kimataifa 49:10 na mengine mengi.

Hivyo basi ni muhimu kuisoma, kuizingatia na kuifuata Kurani tukufu na hili ni agizo la mtume (s.a.w) pale aliposema

"Yuke asiyekumbuka chochote kwa ghaibu katika Quran tukufu ni kama nyumba isiyokaliwa na watu " (TIRMIDHI)

Tena mtume (s.a.w) alisema "Mwenyezi Mungu hajawahi kutega sikio lake kusikiliza kitu chochote minghairi ya jinsi alivyotega kumsikiliza Mtume (s.a.w) kwa shauku anavyosoma Qurani kwa sauti nzuri na ya juu" BUKHAAR/ MUSLIM

Tena anasema "Mtu asiyesoma Quran kwa sauti nzuri hayuko kati yetu" ABUU DAUD

"Mbora wenu ni yule anayejifunza na kuifundisha Quran" BUKHAAR

Atakayesoma aya 10 za Al-BAQARA shetai hataingia nyumbani mwake, nazo ni 4 za kwanza, Ayatul Qursiy na 2 zinazo na 2 zinazofuata na aya 3 za mwisho.

Amma Hadhrat Umar r.a aliwahi kusema kuwa :-

"Amma nabii wenu (s.a.w) amekwisha sema, "Hakika Mwenyezi Mungu atawanyanyua watu kwa kitabu hiki (yani Quran tukufu) na kwacho wengine wataanguka" (SAHIH MUSLIM JUZU YA 3 BAABU MAN YYAQUMU BIL QUR'AAN) katiak zama za Umar r.a zilifngukiwa katika sehemu zote za waislamu na masomo yaliyofundishwa ni Quran, Hadithi n.k

Naye Hadhrat LABID BIN RABI'A R.A mmoja kati ya watu saba waliokuwa mabingwa wa mashairi katika siku zile za mwanzo mwanzo za Islam na ambaye aliingia katika Uislam, alipotakiwa na Hadhrat Umar r.a kwamba asome shairi lake jipya (alilotunga hivi karibuni) yeye akaanza kusoma Qurani tukufu katika sura ya AL-BQARA. Alipoulizwa sababu ya yeye kufanya hivyo ni nini? Alijibu " Nawezaje kutunga shairi ilhali Mwenyezi Mungu amekwishanifundisha sura Al-baqara na Sura Aal- Imran" (GHABA)

Hii inaonyesha hali ya maswahaba watukufu wa Mtume s.a.w, kwamba wao baada ya kuingia katika Islam waliona hakuna cha maaana na chenye thamani isipokua Qurani tukufu, waliipenda, wakaithamini, wakaisoma na kuifuata, nayo iliwainua katika madaraja ya juu kabisa na leo wanatajwa kwa heshima kubwa na mabilioni ya waislamu ulimwenguni kote.

HADHRAT MASIH ALIYEAHIDIWA A.S

Naye Hadhrat Masihi Mau'uud a.s aliye mwalimu mkuu wa kufundisha Qurani katika zama hizi, ndiye mfano wa pekee katika kuipenda, kuisoma,kuifuata na kuwahimiza wafuasi wake kuifanya hivyo katika vitabu vyake zaidi ya themanini (80) amethibitisha heshima, hadhi , ubora na ukweli wa Qurani tukufu kwa hoja madhubuti kiasi hiki kwamba hajatokea mtoto wa binadamu yeyote kupinga hoja hizo. Akiwahimiza wafuasi wake kuisoma na kuifuata Qurani, Hadhrat Masihi mau'uud a.s alisema :-

"Qurani tukufu ndiyo inayojivuna kuwa ndani yake mna tiba ya maradhi ya aina zote. Mwenyezi Mungu ameandaa ndani yake utaratibu wa kuondoa mabaya yote ya dhahiri . Hivyo basi endeleeni kuisoma na kuitwalii mara kwa mara na fanyeni maombi na jitahidini sana kufanya Maisha yenu yaendane sawa na mafundisho ya Qurani tukufu" (MAL FUDHAAT JALADA LA 3 UK.102)

Tena Masihi aliyeahidiwa a.s amesema:- "Na mafundisho mengine ya bora kwenu ni haya yakuwa msiache Qurani tukufu Ovyo. Kwani ni katika Qurani tu umo Uzima wenu, Basi jihadharini wala msiende hata hatua moja kinyume na mafundisho ya Mwenyezi Mungu na Mwongozo wa Qurani tukufu, Nakuambieni ukweli kuwa mwenye kuvunja hata amri moja ndogo katika amri miasaba (700) za Qurani tukufu, basi yeye kwa mikono yake amefunga mlango wake wa wokovu, HakikaQurani tukufu ndio iliyofungua njia za wokovu wa kweli, uliokamilika na na baki yote ni kama vivuli vyake. Kwa hiyo isomeni Qurani tukufu kwa kufikiria na ipendeni sana, kuoenda ambako hamjakipenda chochote sababu ni kama alivyoniambia Mwenyezi Mungu, "AL-KHAIRU KULLUHU FIL QUR'AN- Heri zote zimo katika Qurani tu. Na hayo ndio ya kweli. Ole kwa watu wanaotanguliza juu yake vitu vingine! Hakika Qurani ndiyo chemchem ya kufaulu kwenu na wokovu wenu wote. Hapana haja ( Mafundisho) yoyote katika haja ( mafundisho) za dini yenu ila mtaipata katika Qurani tukufu. Qurani ndiyo itakayosadikisha au kukadhibisha imani yenu siku ya kiyama. Minghairi ya Qurani hapana kitabu kingine chini ya Mbingu kinachoweza kuwaongozeni. Mwenyezi Mungu amawefanyieni ihsani kubwa kwa kuwapeni kitabu kama Qurani. Basi iheshimuni neema hii mliyopewa. Hii ni neema ipendwayo sana na ni hazina kubwa, lau kama isingelikuwa Qurani, dunia yote ingekuwa kama kipande kichafu cha nyama. Qurani ni kitabu cha mwongozo ambacho mbeke yake mwongozo mwingine si kitu. Watakao iheshimu Qurani, watapata heshima mbinguni. Na watakaoiheshimu Qurani, watapata heshima mbinguni. Na watakaoitanguliza Qurani tukufu kuliko hadithi zote na maneno yote nao watatangulizwa mbinguni. Sikilizeni! Na sasa hapana kitabu chochote kitakachoweza kuongoza mwanadamu juu ya ardhi ila Qurani tukufu. (SAFINA YA NUHU)

Akionya juu ya kwenda mbali na Qurani tukufu Masihi aliyeahidiwa a.s alisema:- "kutengana na Qurani hata kidogo ni maangamio yetu"

Haya ni maelezo mafupi yaliyojaa kila aina ya tahadhari na yenye manufaa makubwa sana kwetu. Hebu na tuwaangalie wenzetu walio nje ya Jumuia hii ni madhila gani wanayapata. Mimi nadhani kila mmoja wetu achukulie kauli hii ya Masihi aliyeahidiwa a.s kama ni dira ya maisha yetu ya kila siku na ya kuikumbuka.

FAIDA YA KUFUATA MAFUNZO YA QURANI TUKUFU KILA SIKU

Kwa kufuata mafundisho ya Qurani tukufu katika maisha yetu ya kila siku, faida nyingi sana zinapatikana, baadhi yake ni kama vile:-

Kupata ukaribu na mola wetu mtukufu kama vike isemavyo Qurani tukufu katija aya hii ifuatayo :- "Hakika wale waliosema mola wetu ni Mwenyezi Mungu na kisha wadumu imara, huwateremkia malaika wakiwaambia msihofu wala msihuzunike, sisi ndiyo walinzi wenu katika maisha ya dunia na katika akhera.

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Mwenendo mwema unaotarajiwa kwa kila Ahmadiyya

*Kutoka uk. 12*

hata kama kwa kufanya hivyo ibidi kunyang'anywa mali yake yote.

Mtume Muhammad s.a.w. alisisitiza sana kwamba Waislamu wote ni lazima wafanye Baiat ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. hata kama iwabidi kutambaa juu ya theluji pale aliposema:
Faidhaa ra aytumuuhu fabaa yi 'uuhu walaw habwan alath thalji fainnahuu Khaliifatullaahil Mahdiyya. Yuqiimun naasa 'alaa millatii wa sharii 'atii wa yad 'uuhum ilaa Kitaabil Laahi 'azza wa jalla. Man atwaa 'ahuu fa qad atwaa 'anii wa man 'aswaahu fa qad 'aswaa anii.

Yaani mtakapomuona Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni lazima mkafanye Baiat yake hata kama itabidi mtambae juu ya theluji, kwa sababu yeye, kwa hakika, atakuwa ni Khalifa wa Mwenyezi Mungu atakayekuwa akiongozwa na Mwenyezi Mungu. Atawaimarisha watu katika mila yangu na sheria yangu na atawaita kwenye Kitabu cha Allah, yaani Kurani Tukufu. Atakayemtii yeye atakuwa amenitii mimi na atakayemuasi atakuwa ameniasi mimi.

Nasaha hizi za Mtume s.a.w. zinaashiria wazi kabisa kuwa katika zama hizi hakuna yeyote atakayekuwa anaufundisha Uislamu halisi isipokuwa Masihi Aliyeahidiwa ambaye atakuwa pia ni Khalifa wa kuteuliwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu, ikiashiria kuwa atakuwa ni Nabii wa Mwenyezi Mungu atakayekuwa chini ya Ukhalifa wa Mtume Muhammad s.a.w., kama mwenyewe Mtume Muhammad s.a.w. alivyowahi kuashiria katika moja ya Hadithi zake pale aliposema kuhusiana na Masihi Aliyeahidiwa atakayekuja kwa lakabu ya Isa mwana wa Mariamu kwamba: Alaa innahuu Khaliifatii fii ummatii yaani Fahamuni kwamba kwa hakika yeye huyo Isa mwana wa Mariamu atakayetokana na Waislamu akiwa Imamu wao, atakuwa ni Khalifa wangu atakayetokana na umati wangu.

Kama nimevyosema, kwamba mara kadhaa Mtume Muhammad s.a.w. alishatahadharisha kwamba umati wake utagawanyika katika makundi 73 ambayo yote yatakuwa ni ya upotoshaji na yenye kuelekeza motoni isipokuwa kundi moja tu ambalo litakuwa na mwenendo halisi wa jinsi alivyokuwa yeye na masahaba zake. Hakuna shaka yoyote ile kuwa kundi hilo ni lazima litakuwa kundi lile lililoanzishwa na mtu yule aliyetusisitizia sana tushikamane naye na kufanya Baiati yake, ambaye atafanikishwa na Allah kuistawisha nidhamu ya Ukhalifa kama ule wa awali uliojumuisha pia Makhalifa wenye madaraja ya unabii, kama ibainishwavyo na Sura ya Almaida aya 45 pale Mwenyezi Mungu Aliposema:

Hakika Tuliteremsha Taurati yenye mwongozo na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha kwa Allah waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia, kwa sababu walitakiwa kukihifadhi Kitabu cha Allah.....

Maadam Kurani Tukufu pia imeahidiwa kuhifadhiwa, basi ujio wa Makhalifa wa aina hii ni lazima pia utokee ndani ya Islam, ambapo Makhalifa wenye madaraja ya unabii na mengineyo watadhihiri na kusimamia vema kazi ya kuihifadhi Kurani dhidi ya mashambulizi ya nje na ndani ya wafuasi wa Ibilisi, kwa kufunuliwa wahyi wa mafundisho sahihi na hoja madhubuti zisizopingika.

Katika zama zetu hizi amedhihiri Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadian na kuitangazia dunia kwamba yeye ametumwa na Mwenyezi Mungu akiwa nabii yule aliyeahidiwa kufika katika siku za mwisho kwa lakabu ya Isa bin Mariam, Imam Mahdi, Masihi Aliyeahidiwa, ili kuirejesha dunia kwenye dini ile ya asili iliyokuwa ikifundishwa na manabii wote na kuja kukamilikia kwa Mtume Muhammad s.a.w.

Aliwaasa wanadamu wafanye Baiat yake na kumuamini na kumfuata ili awaongoze kwenye ucha Mungu wa kweli. Alisema:

"Hii Baiat, maana yake ya asili ni kujiuza. Baraka na athari zake zimeambatana na sharti lile lile kama la mbegu iliyopandwa ardhini. Hivyo hali yake ya mwanzo huwa hivi hivi kama ile mbegu iliyopandwa na mkulima ambayo haijulikani kwamba sasa itakuwa nini. Lakini kama mbegu hiyo ni bora na ndani mwake mna nguvu ya kustawi, basi kwa fadhili za Mwenyezi Mungu na jitihada za mkulima huyo, (mbegu) hiyo huchipua, na punje moja hugeuka kuwa punje nyingi sana.

"Halikadhalika mtu afanyaye Baiat, kwanza hulazimika kuwa mnyenyekevu na kuachana na kujipenda na ubinafsi. Hapo ndipo anakuwa mwenye uwezo wa kustawi. Lakini yule aliyefanya Baiat na kuendelea kuwa mbinafsi, huyo hatapata baraka asilan. (Malfudhaat jal. 6 uk. 173).

Tena anasema:

"Mradi wa Baiat ni kuikabidhi nafsi kwa Mwenyezi Mungu. Mradi wake ni huu kwamba, leo sisi tumeiuza nafsi yetu kwa Mwenyezi Mungu. Hii si sahihi asilan kwamba hatimaye mtu anaweza kupata hasara kwa kutembea katika njia ya Mwenyezi Mungu. Mkweli hawezi kamwe kupata hasara. Hasara ni ya yule aliye mwongo, avunjaye Baiat na ahadi aliyoifunga na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya dunia. Mtu yule atekelezaye mambo hayo kwa ajili tu ya kuihofia dunia, basi na akumbuke kwamba wakati wa mauti hakuna mtawala wala mfalme yeyote atakayeweza kumuokoa. Yeye ni mwenye kwenda tu kwa Hakimu wa mahakimu wote, Atakayemuhoji kwamba kwa nini hukunijali? Hivyo ni muhimu kwa kila mwaminio kwamba amuamini Mwenyezi Mungu Aliye Mmiliki wa Mbingu na Ardhi na afanye toba ya kweli." (Malfuudhaat jal. 7 uk. 29 – 30).

Akifafanua zaidi, Hadhrat Khalifatul Masih V atba. Anasema:

"Muhtasari wa masharti kumi ya Baiat ni kwamba kila mmoja wetu alifahamu jambo hili kwamba dhati yake sasa sio tena dhati yake, bali kuanzia sasa anapaswa kushikamana, kwa hali yoyote ile, na maagizo ya Mwenyezi Mungu kwa kuyafuata, na kila tendo liwe kwa ajili tu ya kuipata ridhaa ya Mwenyezi Mungu."

Kufanya Baiat si tendo la uzushi kama baadhi ya Waislamu wanavyodhani, bali hiyo ilikuwa ndio desturi ya kusilimu wakati wa Mtume Muhammad s.a.w. Kuna riwaya iliyosimuliwa na Hadhrat Aidhullah bin Abdullah isemayo:

"Ubada bin Swaamit alikuwa ni miongoni mwa wale Masahaba walioshiriki katika vita vya Badri na aliyeshiriki katika Baiat ya Uqba. Ubada bin Swaamit alimwambia kwamba Mtume s.a.w. alilisema jambo hili katika wakati ule alipokuwa amezungukwa na kundi fulani la masahaba, kwamba 'Njooni mfanye Baiat yangu kwa sharti hili kwamba:

Yaani hamtamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hamtaiba, wala hamtazini, wala hamtawaua watoto wenu, wala hamtazua uzushi na wala hamtaniasi katika jambo lolote lililo jema.

'Basi miongoni mwenu atakayetimiza ahadi hii ya Baiat basi ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Na yule atakayelegea katika kuitimiza ahadi hii na akapata adhabu humu humu duniani, basi adhabu hiyo itakuwa ni kafara kwa ajili yake. Na yule aliyelegea katika kuitekeleza ahadi hii ya Baiat, halafu Mwenyezi Mungu Akamsitiri basi shauri lake liko mkononi mwa Mwenyezi Mungu. Akipenda anaweza kumuadhibu au kumsamehe.
(Sahih Bukhari – Kitabu manaqibul – Ansaari – Baab Wufuudul Ansaari Ilan Nnabiyyi Bimakata Rabiat – ul – Uqbatu.)

Kuna Hadithi nyingine iliyosimuliwa na Hadhrat Ubaidah bin Saamit aliyesema kwamba:

"Sisi tulifanya Baiat kwa Mtume (S.A.W) kwa sharti hili kuwa tutasikia na kutii katika hali ya faraja na dhiki, au katika furaha au huzuni, na wala hatuta gombana na wenye mamlaka juu yetu. Na popote tutakapokuwepo tutadumu katika haki na hatutaogopa lawama ya yeyote mwenye kulaumu.
(Bukhari kitabul-Baiati babul Baiat alas sam'i wattaati)

Umul Mu'mimin Hadhrat Aisha r.a anasimulia kuwa Nabii Mkarim (S.A.W) alikuwa akichukua Baiat ya wanawake kulingana na aya hii tukufu:-

Yaani; Ewe Nabii! watakapokujia wanawake waliosilimu na kutaka kufanya Baiat katika sharti hili kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawauwa watoto, wala hawatamzushia yeyote uzushi, wala hawatakuasi katika mambo mema, basi pokea Baiat yao na uwaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mrehemuvu. [Sura 60 Almumtahana aya 13]

Hadhrat Aisha (r.a) anasimulia kuwa Mtume (S.A.W) alipokuwa akichukua baiat, mkono wake wenye baraka ulikuwa haugusi mkono wa mwanamke yeyote isipokuwa mwanamke aliyekuwa ni mke wake.
(Sahih Bukhari – Kitaabul – Ahkaami – baabu Baiatin Nisa-i)

Kwa hiyo tumeona hapa kwamba hata Mtume Muhammad s.a.w. alitilia mno maanani suala la Baiat jambo linalothibitisha umuhimu wa kufanya Baiat na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. alieleza umuhimu wake kwa ufasaha zaidi pale aliposema kwenye tangazo lake la tarehe 4 March, 1889 la huko Ludhiana kwamba:

"Mfumo huu wa Baiat umeanzishwa tu kwa ajili ya kuwakusanya wacha Mungu katika Jumuiya ili kundi kubwa la wacha Mungu litoe athari yake njema duniani. Umoja wao uwe chimbuko la baraka na taadhima na matokeo mema kwa ajili ya Islam. Na kutokana na kuafikiana kwao juu ya Kalima moja yenye baraka waweze kutumika kwa haraka katika kutoa hudumu tukufu za Kiislamu na wasiwe Waislamu wavivu na wabakhili wasiokuwa na faida yoyote. Wala wasiwe kama wale watu wasiokuwa na thamani walioleta madhara makubwa kwa Islam kutokana na kutoafikiana kwao na kufarakana na wakatia doa kwenye uso mzuri wa Islam kutokana na hali zao za kifasiki. Na wasiwe kama wale Madaruweshi walioghafilika na wale watu waliojitenga kabisa na dunia wasio na habari yoyote juu ya mahitajio ya Kiislamu na wasio na huruma yoyote kwa ndugu zao na hawana ari yoyote ya kuwanufaisha wanadamu, bali wawe ni wenye kuwahurumia watu kiasi hiki kwamba wawe ni kimbilio la masikini, wawe mababa kwa ajili ya mayatima na wawe tayari kujitoa muhanga kama yule aliyehemewa na mapenzi katika kuuhudumia Uislamu, na wafanye juhudi yote kwa ajili ya jambo hili kwamba baraka zao za kawaida zienee duniani na chemchem takatifu ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na huruma kwa waja wa Mwenyezi Mungu itoke katika kila moyo na kujumuika sehemu moja na kuonekana ikitiririka katika sura ya mto utiririkao.

"Mwenyezi Mungu Anataka kuanzisha kundi hili na kulipatia mafanikio kwa ajili ya kudhihirisha ujalali wake na kuonyesha Kudra yake ili Aeneze mapenzi ya Mungu, toba ya kweli, utakaso, wema wa kweli, amani, suluhu na huruma kwa binadamu duniani kote. Hivyo kundi hili litakuwa ni kundi lake makhsus Naye Mwenyewe Atawapa nguvu kwa roho Yake na Atawalinda na maisha machafu na Ataleta mabadiliko matakatifu katika maisha yao na kama vile Alivyoahidi katika bishara zake takatifu kwamba Atalikuza sana kundi hili na Atawaingiza maelfu ya wakweli ndani ya kundi hili na Mwenyewe Atalilea kundi hili na kulistawisha kiasi ya kwamba uwingi wao na baraka zao zitawastaajabisha watazamaji, na wataeneza nuru yao pande zote nne za dunia kama ile taa iliyowekwa mahali pa juu nao watakuwa kama mfano wa baraka za Kiislamu.

"Atawapa ushindi wa baraka za kila aina, wafuasi kamili wa Jumuiya hii, dhidi ya watu wa silsila zingine na daima hadi Kiama watapatikana watu miongoni mwao watakaopewa msaada na kukubalika. Mwenyezi Mungu huyu mwenye shani Ametaka hivi hivi, Yeye ni Mweza, Hufanya Atakacho. Kila nguvu na uwezo vi Kwake."

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Baraka za Ukhalifa katika zama hizi

*Kutoka uk. 12*

yakihitaji nidhamu maalum na juhudi endelevu, na kwa kuwa umri wa mtume unakuwa na kikomo chake, hivyo kutokana na sunna Yake, Allah Subhanahu wa Taala baada ya kufariki kwa mtume huyo Anamteua mwakilishi wake na hivyo Hutimiza shabaha ya kumleta mtume huyo duniani, mwakilishi huyo katika istilahi ya Kiislamu anakumbukwa kwa jina la Khalifa Mtukufu, ambalo maana yake ni mtu anayemfuata mwingine na kuchukua nafasi yake.

Ndugu wasikilizaji, mitume wa Allah huwa ni waja Wake walio bora na wema zaidi kushinda wengine, hivyo ili Baraka zao zibaki duniani milele na dunia isikose Baraka za utume, Allah Subhanahu wa Taala Anasimamisha ukhalifa duniani. Ukhalifa huo umeendelea kupatikana tangu awali kama asemavyo Bwana wetu Mtukufu saw ya kuwa:

"Hamna katu Unabii isipokuwa Ukhalifa uliufuata".

Hivyo baada ya kufariki kwa Hadhrat Musa as Yoshua alichaguliwa kuwa Khalifa na baada ya Hadhrat Issa as, Pilato akawa khalifa wake na alipofariki mtume wetu mtukufu saw, Allah Alimfanya Hadhrat Abu Bakr Siddiq ra kuwa Khalifa wa kwanza, bali niseme ya kuwa baada ya mtume wetu mtukufu nidhamu hii ya ukhalifa ilipatikana ikiwa na shani yake pekee ikilinganishwa na ukhalifa wa mitume wote waliopita kabla yake.

Seyydna Ahmad as akielezea uanzishwaji wa nidhamu hii ya khilafat e Rashida katika enzi za Mtukufu Mtume saw alisema kuwa 'wakati huo kifo cha Mtume saw kilipofikiriwa kutokea katika wakati usiofaa na mabedui wengi wakaritadi na masahaba kwa sababu ya huzuni kubwa wakawa kana kwamba wameshikwa na wazimu, hapo Mwenyezi Mungu kwa kumsimamisha imara Hadhrat Abu Bakr Siddiq ra Akaonesha mara ya pili onesho la kudra yake na Akanusuru Islam iliyokurubia kufutika na Akatimiza Aliyoahidi ya kuwa (aya)

Yaani, baada ya hofu Tutawaimarisha,

Ndugu zanguni historia ni shahidi ya kuwa katika miaka hii thelathini ya Ukhalifa Islam ilienea kote kote na kuimarika kiasi hiki ya kuwa wafalme wakubwa wakubwa kwa kusikia jina la Khalifa walikuwa wakitetemeka, tena katika enzi hiyo ya Ukhalifa Islam ilipata ushindi ulio dhahiri na baadhi ya bishara zilizotolewa na Mtukufu Mtume saw zikapata kutimia zisemazo kuwa nimepewa funguo za kaisari wa Roma na kisra wa Irani, madola haya makuu yakatekwa na Waislamu na bendera ya Islam ikapeperushwa huko.

Kisha kutokana na bishara itolewayo na mtume saw isemayo (Arabic)

Yaani kisha utapatikana Ukhalifa juu ya njia ya Unabii, basi Mwenyezi Mungu Alimtuma Masihi na Mahdi wa Mtume Muhammad saw akimfanya kuwa nabii mfuasi wake katika aakhariina na kumwita katika wahyi kwa jina la khatamul khulafaa. Basi muda uliwadia ambapo uislamu uliokuwa umebaki kwa jina tu ukahuishwa, na kurani iliyokuwa imebaki maandishi ikafuatwa tena na wafuasi wake na dini kwa jumla iliyokuwa ikitungikwa kwenye kilimia ikaletwa mara nyingine tena duniani, giza lilitoka na nuru ikachukua nafasi yake, ukweli ulifika na uongo ukatoweka, na nuru ya mtume Muhammad saw ikasambaa duniani.

Kisha baada ya kufariki kwa masihi mauud as Mwenyezi Mungu Aliineemesha jumuiya yake kwa kudra ya pili, furaha bandia za maadui zilikanyagwa mbali na neema ya Ukhalifa ikaletwa tena na Allah na ahadi yake ya kuleta ukhalifa kati ya waumini ikatimia kwa shani yake yote na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya chini ya uongozi wa mmoja baada ya mwingine iliendelea kupata maendeleo juu ya maendeleo hapo historia yetu ya Ukhalifa ya miaka mia moja na sita ni shahidi na inatangaza kinaga ubaga kuwa ahadi zote za Allah zilizoahidiwa katika aya ya Ukhalifa zimeendelea kutimia mara kwa mara na leo chini ya uongozi wa Khalifa Mtukufu wa Tano Jumuiya inaendelea kusonga mbele na mbele.

Ndugu wapenzi katika zama hii ya leo sababu kuu ya ukosekanaji wa utulivu na amani ni kukosa mwongozo, takriban katika bara zote ufisadi umekwishatokea, maafa na masaibu yamekithiri sana, dunia inaelekea kwenye vita kuu ya tatu, mabalaa yanayotokea ardhini na mbinguni yamejumuika kwa pamoja, katika hali kama hiyo enyi wanadamu furahini ya kuwa katika majanga hayo mkombozi wenu amekwishafika tayari (Shairi)

Na leo Khalifa wake wa Tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.h.t kwa kutukomboa sisi toka majanga hayo yote anatufurahisha na kutangaza kwa maneno ya Masihi Mauud ya kuwa (shairi)

Hali ya dunia ni tete kwa wale wasiokuwa na Ukhalifa na ni wazi mbele yetu, ingawaje hao wote huelewa na kukubali kuwa utatuzi wa matatizo yao umo katika uongozi mmoja nao ni Ukhalifa, ndiyo sababu ya kuwa katika nyakati tofauti walijaribu kuleta Ukhalifa kati yao, lakini wakati wote walishindwa katika mpango wao, iwe njama itengenezwayo na mfalme wa Saudia Shah Faisal au iwe ndoto ya Rais wa zamani wa Pakistan kujifanya kuwa Amir ul muuminiin au taasisi iliyopatikana juzi juzi ya Daaish huko Iraq, kila atakayekuja mbele ya Ukhalifa wa Allah atasagwa na kufanywa kuwa vipande, kwani Ukhalifa uliosaidiwa na Allah umekwishapatikana.

Hadhrat Khalifa tul Masihi wa pili ra alisema kuwa; kudra ya pili ilipatikana na kudhihirika lakini ni jambo la kusikitisha ya kuwa, wapo wengi wasioitambua. Mimi nikisimama mahala popote patakatifu pa dunia kwa kuapa kwa Allah naweza kusema kuwa kudra ya pili iliyokuwa ikitabiriwa imekwishadhihirika na hii ndiyo njia pekee ya kupata ushindi na maendeleo ya Islam duniani.

Ndugu wapendwa, leo huu ni ukhalifa wa kiahmadiyya tu unaoweza kuleta mabadiliko na mapinduzi ya kweli, syedna Hadhrat Musleh Mauud ra alisema; kumbukeni ya kuwa maendeleo yenu yote yamo katika kujiunga na Ukhalifa na siku ambapo mkisahau jambo hili na kughafilika nalo basi siku hiyo itakuwa siku yenu ya mwisho, lakini endapo mtaendelea kushikamana na Ukhalifa basi lau kama dunia nzima itaamua kuwaangamiza nyinyi haitaweza kufanya chochote.

Chaudhry sir Muhammad Zafar ullah Khan Sahib, ni nani asiyemjua mtumishi huyu wa Jumuiya? Yeye alipata mafanikio mengi katika maisha yake, siku moja alipoulizwa kuwa kuna siri gani iliyopo nyuma ya maendeleo hayo, akasema; sijui mengi lakini katika maisha yangu yote nimekuwa mtiifu wa Khliafat e Ahmadiyya.

Katika zama za leo dunia imekosa amani na utulivu, siku hadi siku dunia inakwenda kuporomoka na kuanguka kwenye shimo la upotevu, viongozi wa dunia wameshasahau maadili na wengine wanaojidai kuwa manahodha wa safina ya Islam, hawaijui maana ya neno la Islam, shingo zinakatwa kwa jina la jihadi, mauaji yameongezeka, uadilifu umekuwa maneno ya mdomoni tu, dhuluma imezidi na hayo yote hufanywa kwa jina la Allah.

Upande wa pili wapinzani wa Islam pia hawaachi hata dakika moja kutumia fursa hii kwa kuishambulia Islam, heshima ya mtume wetu inachafuliwa, na picha ya Islam ioneshwayo na hao wadhalimu ni ile dini ya ugaidi inayowapa wafuasi wake somo la kuleta ufisadi duniani.

Ndugu Waahmadiyya katika hali hii ya kutisha tuangaliapo, tunamkuta mtu mmoja tu akiwa anaongoza jumuiya yake naye ni Khalifa tul Masihi wa Tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.h.t.

Leo kwa kupitia ukhalifa wake mapinduzi ya kiroho na ya kweli yamepatikana hapa na pale na bilkhususi dunia ya kiahmadiyya na kwa jumla dunia nzima inaendelea kupata Baraka na mabadiliko ya kweli na hayo yote ni Baraka za Ukhalifa na silsila hiyo ni endelevu tangu siku ya kwanza, ndugu waahmadiyya mpaka leo mti huu wa jumuiya umekwishapandwa katika nchi mia mbili na sita na jumuiya kustawi humo na wanajumuiya wa nchi hizo hutangaza kwa sauti moja ya kuwa enyi mnaotazama tazameni ya kwamba chini ya uongozi wa makhalifa wa jumuiya msafara huu wa kiroho waendelea kusonga mbele na leo kwa fadhila ya Allah katika pande zote za dunia waumini wa jumuiya wapo, iwe ardhi ya visiwa vya Fiji au Morisi, Norwe au Irelandi, Japani au Aljeria, iwe Afrika Mashariki au Magharibi, kusini au kaskazini tunaona mandhari ya ardhi kung'aa kwa nuru ya Mola wake.

Tuelekeapo bara la Afrika, basi niwaambieni hali ya wanajumuiya wa huko ielezwayo na Bwana Abdul Majid Tahir Sahib wakil tu tabshir aliyebahatika kusafiri pamoja na Huzur Anwar, wakati wa mkutano wa mwaka nchini Ghana uliofanyika mwaka2008, yeye anasema, wakati wa mkutano huo Huzur alikaa kwenye uwanja wa Jalsa ambapo watu takriban laki moja walikuwa wamehudhuria na toka nchi zingine za Afrika pia wanajumuiya walikuwa wakifika, baada ya kipindi cha Jalsa khalifa Mtukufu alipokuwa akirudi nyumbani kwake basi njia zilikuwa zikifurika na watu kwa pande zote mbili, gari ya Huzur ilikuwa inaenda pole pole, kinamama walikuwa wakipeperusha vitambaa vyeupe na kuonesha mapenzi yao kwa Khalifa, watu walikuwa wanapiga takbira kwa shauku, jazba na mapenzi ya hali ya juu ya kuwa sauti nyingine hazikusikika.

Kila mmoja wao alikuwa anajisogeza mbele ili aweze kumwona khalifa wao kwa karibu, baadhi ya mama walibeba watoto wao kwenye mabega yao kwamba khalifa wao awaone kwa karibu nao pia wapate Baraka hizo, hayo ni mapinduzi yale ya kweli yatokanayo na Baraka za ukhalifa wa kiahmadiyya peke yake. Kisha katika mkutano huu wa Ghana makhuddam mia tatu walikuja toka Burkina Faso, vijana hao walisafiri na baiskeli zao, safari ambayo ilikuwa ya kilomita 1600. Miongoni mwa hao mlikuwa watoto wawili wa miaka 13, watoto hao walipofahamishwa ugumu wa safari ile wakaanza kulia na kusema kuwa wanatamani kwenda kumwona khalifa wao hivyo wako tayari kukabiliana na ugumu wa aina yoyote basi nao pia wakaruhusiwa kuwa sehemu ya msafara huo.

Baada ya kufika kwa ujumbe huo Sadr Sahib Khuddamul Ahmadiyya Burkina Faso alipoulizwa sababu gani iliwafanya wachague kazi hii ngumu akasema ya kuwa, sisi tulikuwa tunamhakikishia khalifa wetu ya kuwa vijana wako wanakupenda sana na wapo tayari katika kujitolea kila kitu kwa ajili ya ukhalifa.

Siku moja wanajumuiya watokao nchi hizi za Burkina Faso na Ivory Coast wanajumuiya elfu nne walibahatika kukutana na Khalifa Mtukufu, baada ya kumsalimia Huzur, walikuwa wakipaka mikono yao kwenye nyuso zao na vifua vyao na kusema ilhali machozi yakitiririka machoni mwao kwamba leo moyo wetu umejaa na Baraka, sisi ni watu wenye bahati ya namna gani ya kuwa leo tumemshuhudia khalifa wetu kwa macho yetu. Mtu mmoja alisema huyu ni nuru kabisa, watu hao waliotokea mbali sana kwa kumwona khalifa mbele yao walisahau uchovu wao, kwani uchovu huo ulikuwa hauna thamani yoyote mbele ya furaha yao.

Kisha katika nchi za Uarabuni kwa fadhila na msaada wa Allah mapinduzi ya ajabu yametokea humo, hali ndiyo hii kwamba hamna siku hata moja ambapo baiati zisipatikane toka nchi hizi za Uarabuni, wengi wao wanajiunga na jumuiya kwa kushuhudia miujiza ya Ukhalifa, mfano wake ndio huu ya kwamba mama mmoja wa Aljazaair aliyekuwa bado mwanajumuiya mpya alipokutana na Huzur, akamwomba Huzur afanye maombi kwa ajili ya mamake aliyekuwa akiuguwa maradhi ya kansa, hapo Khalifa Mtukufu akamwombea na kunena kuwa, Allah Atamponya na kumletea fadhila yake, pia Huzur akampa pete iliyokuwa na maandishi ya AALAISALLAHU BIKAAFIN ABDAHU ambayo mamake alivaa kwenye kidole chake. Baada ya siku chache mama yake alipoenda kwa ajili ya kupimwa, daktari akampima na kupigwa na butwaa naye akanena ya kwamba mama huyu hahitaji kipimo chochote kingine au chemotherapy kwani siha yake ni bora zaidi kuliko wakati ule ambapo alikuwa bado hakupata maradhi haya ya kansa. Tukio hili lilibadilisha moyo wa familia yake na kwa kuona muujiza huo wa Ukhalifa watu 36 wa familia hiyo wakafanya baiati na kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya.

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

# MapenziyaMungu

Dh.Hij/ Muhar. 1435/36 AH | Okt./Nov. 2014 | Tabk/Nubw. 1393 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w**

**Imesimuliwa na Hadhrat Zaid bin Thabit r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Salini katika nyumba zenu, kwani sala bora ya mwanamume ni ile anayosali nyumbani mwake isipokuwa sala ya faradhi inayosaliwa pamoja kwa jamaa. (*Masnad Darmii*).**

# Baraka za Ukhalifa katika zama hizi

*Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2014 na Sheikh Waseem Ahmad Khan*

Waheshimiwa wasikilizaji mliojaaliwa kuhudhuria mkutano huu muhimu na adhimu,
Assalaam alaikum warahamtullah wabarakaatuh.

Mada niliyopangiwa kuizungumzia siku hii ya leo ni muhimu sana, nayo ni Umuhimu na Baraka za Ukhalifa katika zama hizi.
Allah Subhanahu wa Taala Anasema katika kitabu chake kitakatifu ya kuwa (aya)

Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka yoyote Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa




*Sheikh Waseem Ahmad Khan akitoa hotuba kwenye Jalsa Salana (mkutnao wa mwaka) wa 45, uliofanyika Kitonga Dar es Salaam*

yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo yaani baada ya kuwepo kwa nidhamu hiyo ya Ukhalifa, basi hao ndio wavunjao amri.
Ndugu zangu wapendwa, kwa kupitia mafundisho ya kurani Tukufu na historia ya mitume, tunapata kuelewa kuwa Mwenyezi Mungu Atumapo mtume Wake basi shabaha yake inakuwa siyo hii tu kwamba mtume huyo kwa kufika duniani awe awatangazie watu mara moja na kuwaambia kuhusu mwumba wao na kurudi kwa Mola wake, bali katika zama yake mpango wa Allah upangwao na Yeye unakuwa ni wa kuleta mabadiliko na mapinduzi ya kiroho katika maisha watu wale, ambayo yanakuwa

*Endelea uk. 11*

# Mwenendo mwema unaotarajiwa kwa kila Ahmadiyya baada ya kufanya baiat kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

*Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2014 na Sheikh Bakri A. Kaluta*

Allah Amewaahidi wale walioamini kati yenu na kufanya vitendo vizuri kwamba Atawafanya Makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao. Na Atawaimarishia dini yao Aliyowaridhia na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu Mimi tu, hawatanishirikisha na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri.

Aya hii yaashiria kwamba Waislamu watakaoweza kuiimarisha Islam na hivyo kujaaliwa utulivu wa moyo na amani baada ya hofu, watakaokuwa wakifanya ibada ya kweli isiyo na shirki ndani yake, watakuwa ni wale watakaokuwa ndani ya nidhamu ya ukhalifa unaoshabihiana na ukhalifa ule wa hapo awali. Yaani kama hapo awali walipatikana makhalifa wenye madaraja ya unabii, basi wao hawataikana neema hiyo ya kudhihiri tena ndani ya Islam. Na waislamu wote watakaoikana neema ya



*Sheikh Bakri Abedi kaluta akitoa hotuba kwenye Jalsa Salana (mkutnao wa mwaka) wa 45, uliofanyika Kitonga Dar es Salaam*

ukhalifa wa unabii kudhihiri tena ndani ya Islamu na wale watakaojitenga na ukhalifa ule utakaochipukia ndani ya unabii, hao wote watahesabiwa kuwa ni waasi wavunjao amri, kwani hata Mtume Muhammad s.a.w. alishabashiri kwamba Ukhalifa wa njia ya wazi ya unabii utatokea tena katika siku zijazo.

Miongoni mwa bishara alizotoa Mtume s.a.w. ni zile za kuporomoka kiimani kwa Waislamu pale aliposema Saya atii zamaanun laa yab qaa minal Islaami illasmuhuu, walaa yabqaa minal Quraani illaa rasmuhuu, masaajiduhum ‘aamiratun wa hiya kharaabum minal hudaa, ‘ulamaauhum sharru man tahta adiimis samaai, min ‘indihim takhrujul fitnah wa fiihim ta’uud. Yaani itafika zama ambapo Islamu haitabakia kitu ila jina lake tu, na Kurani haitabakia kitu ila maandishi yake tu, misikiti yao itakuwa mikubwa iliyojaa lakini itakuwa na miongozo iliyoharibika, masheikh wao ndio watakuwa waovu kuliko wote waliomo chini ya mbingu, fitina itaanzia kwao na kuwarejea wenyewe.

Pia aliwahi kusema: Taftariqu ummatii ‘alaa thalaathin wa sab’iina millatan, kulluhum fin naari illaa millatan waahidatan yaani umati wangu utagawanyika katika makundi sabini na tatu ambayo yote yatakuwa ya motoni isipokuwa kundi moja tu. Alipoulizwa ni kundi lipi hilo, akajibu ni lile litakalokuwa juu ya mwenendo wangu na wa masahaba zangu.

Sehemu nyingine alimwambia Hadhrat Hudhaifa bin Yaman r.a. kwamba itafika zama fulani ambapo watapatikana masheikh watakaokuwa wakijinasibisha na uislamu kwa mavazi na kauli, lakini watakuwa wakifundisha yaliyo kinyume na mafundisho ya Mtume s.a.w. Hivyo akamnasihi Hadhrat Hudhaifa kwamba wakati huo ajiepushe kabisa kushikamana na madhehebu tofauti yatakayokuwa yanaongozwa na masheikh hao waovu, hata kama itabidi akimbilie porini na kula mizizi ya miti. Bali alimtaka aitafute Jumuiya ya Waislamu itakayokuwa inaongozwa na Imamu mmoja mwenye lakabu ya Khalifa,

*Endelea uk. 10*